
Haliuzwi
MEI 18, 2026
/islamicftz
Dhul-Hijja 1 1447
# IMAAN
ISSN 5618 - NO. 583
Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

## Aref Nahdi: Wahitimu Forest Hill mkawe mabalozi wa Uislamu



# Uganda yatimiza ndoto ya Sukuk za Serikali Afrika Mashariki

■ Yakaribisha wawekezaji wa Tanzania kushiriki katika Sukuk yake ya kwanza ya serikali ya euro milioni 405 (Sh trilioni 1.2) kugharimia ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR kutoka Malaba hadi Kampala.






## Balozi wa Palestina afichua hali halisi ya mateso Gaza



## Mfalme Salman atuzwa kwa kuunga mkono hifdh ya Qur'an

## Tusiigeuze ibada ya hijja kuwa 'outing'



## Kama Tanzania, Kenya nako 'twisheni' shule za academic zapora muda wa madrasa kwa wanafunzi







MUDA WA ZIADA MASOMO KUPITA RATIBA RASMI

### ATHARI KWA MWANAFUNZI WA KIISLAMU

- Kukosa muda wa masomo ya Madrassa
- Hupunguza muda wa kujifunza Qur'an na Dini
- Kupoteza Baraka ya muda na malengo ya Dini




المؤسسة الإسلامية
The Islamic Foundation
KICHINJO CHA MBUZI KWA AJILI YA
Eid Al-Adha
Bei ya MBUZI ni Shilingi
180,000
GHARAMA ZOTE MPAKA KUMFIKIA MLENGWA
MIXX BY YAS
Lipa kwa Simu
Lipa namba:
15441517
Jina la wakala:
The Islamic Foundation
Kwa Mawasiliano Zaidi:
0716 542 323

NA MWANDISHI WETU

# Sukuk ya Uganda yaashiria zama mpya fedha za Kiislamu Afrika Mashariki

Uganda ipo katika hatua za mwisho za kutoa sukuk yake ya kwanza ya taifa yenye thamani ya euro milioni 405 sawa na zaidi ya Sh trilioni 1.2 za Tanzania kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa reli ya kisasa ya Standard Gauge Railway (SGR) yenye urefu wa kilomita 272 kutoka Malaba mpakani mwa Kenya hadi Kampala.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa wakati wa mkutano wa wawekezaji katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), sukuk hiyo pia ina green shoe option ya euro milioni 45 endapo mahitaji ya wawekezaji yataongezeka zaidi ya kiwango kilichopangwa.

Hatua hiyo inatajwa kuwa muhimu kwa maendeleo ya fedha za Kiislamu Afrika Mashariki huku Uganda ikitarajia kutumia sukuk hiyo kufadhili asilimia 15 ya euro bilioni 2.702 zinazohitajika kwa ajili ya mradi huo wa reli. Asilimia 60 nyingine zinatarajiwa kutoka taasisi za mikopo ya mauzo ya nje (Export Credit Agencies) na asilimia 25 kutoka taasisi za maendeleo ya kifedha (DFIs).

Patrick Ocailap, ambaye ni Naibu Katibu wa Hazina wa Uganda, aliwasilisha fursa hiyo kwa wawekezaji wa Tanzania na madalali wa soko la mitaji wakati wa mkutano maalum wa Non-Deal Roadshow uliofanyika DSE.

Msafara huo pia ulihusisha Benki ya Uganda, Stanbic Bank, Salaam Bank Uganda pamoja na kampuni ya Tanzania ya Yusra Sukuk ambayo ni mshauri mkuu wa muamala huo.

Mwenyekiti Mtendaji wa Yusra Sukuk Company Limited, Sheikh Issa Mohamed, alisema tayari kampuni hiyo imefanya mazungumzo ya mtandao na karibu wawekezaji 25 kutoka nchi za Ghuba (GCC) pamoja na zaidi ya wawekezaji wengine wa kikanda.

"Kwa sasa tunaendelea na maonesho ya uwekezaji Afrika Mashariki na baadaye mwezi huu tunatarajia kwenda Kuala Lumpur nchini Malaysia kabla ya kuelekea Afrika Kusini kwa mazungumzo zaidi na wawekezaji," alisema.

Kwa mujibu wa maafisa wa Uganda, sukuk hiyo itatolewa kwa awamu mbili. Awamu ya ndani na kikanda itakuwa euro milioni 205 pamoja na green shoe option ya euro milioni 30, huku awamu ya kimataifa ikiwa euro milioni 200 pamoja na nyongeza ya euro milioni 15.

Toleo hilo, ambalo linatarajiwa kuzinduliwa kimataifa mwishoni mwa Juni 2026, litatolewa kupitia kampuni maalum ya serikali iitwayo Uganda Treasury Sukuk1 Limited.

Sukuk hiyo pia inatarajiwa kuorodheshwa katika masoko mbalimbali ya fedha duniani ikiwemo Johannesburg Stock Exchange (JSE), Luxembourg Stock Exchange, Nasdaq Dubai, London Stock Exchange pamoja na Bursa Malaysia.

Uganda inaamini mfumo huo utaisaidia kupata fedha za muda mrefu bila kutegemea sana mikopo ya kawaida ambayo imeendelea kuwa ghali kutokana na ongezeko la viwango vya riba duniani.

Sukuk ni mfumo wa kifedha unaofuata misingi ya Shariah ambapo wawekezaji hawapati riba kama ilivyo kwenye bondi za kawaida, bali hupata mapato yanayotokana na mali au mradi halisi unaowekezwa.

Katika mfumo huo, wawekezaji watamiliki sehemu ya mali au miundombinu ya reli na mapato yao yatatokana na matumizi ya mradi huo badala ya riba.


Kwa mujibu wa Uganda, sukuk hiyo imeundwa kwa mfumo mseto wa Forward Ijarah na Istisna. Mfumo wa Ijarah utatoa mapato kwa wawekezaji mara mbili kwa mwaka huku mfumo wa Istisna ukigharamia kazi za ujenzi.

Bw. Ocailap alisema iwapo sukuk hiyo itapata maombi makubwa zaidi ya kiwango kilichopangwa, serikali ipo tayari kuongeza kiwango cha fedha kitakachopokelewa.

"Hatutawakataa wawekezaji wanaotaka kushiriki katika maendeleo ya Uganda," alisema.

Alieleza kuwa sehemu inayotarajiwa kufadhiliwa kupitia sukuk hiyo ni takribani kilomita 42 pekee kati ya kilomita 272 za reli ya Malaba–Kampala, wakati Uganda kwa ujumla inapanga kujenga mtandao wa reli wenye urefu wa kilomita 1,724. Reli hiyo pia inatarajiwa kuunganishwa na Rwanda, Sudan Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) pamoja na mtandao wa reli ya Tanzania kupitia Mwanza na bandari ya Dar es Salaam.

Afisa Mkuu wa Maendeleo ya Biashara wa DSE, Emanuel Nyalali, alisema mpango huo utaimarisha muunganiko wa masoko ya fedha Afrika Mashariki na kupanua bidhaa za uwekezaji katika ukanda huo. Kwa Tanzania, hatua hiyo inaonekana kama ishara mpya ya namna fedha za Kiislamu zinavyoweza kutumika kufadhili miradi mikubwa ya miundombinu bila kutegemea mikopo ya kawaida yenye riba kubwa.



HABARI
DAR ES SALAAM

NA MWANDISHI WETU

# Kama Tanzania, Kenya nao walalamikia ‘twisheni’ kuathiri madrasa kwa wanafunzi

Viongozi wa Kiislamu nchini Kenya wameeleza wasiwasi wao kuhusu baadhi ya shule kuongeza muda wa masomo kupita ratiba rasmi ya serikali, wakisema hali hiyo inaathiri masomo ya madrasa na maendeleo ya kiroho ya wanafunzi wa Kiislamu.

Kwa mujibu wa Eastleigh Voice, Baraza la Maimamu na Wahubiri wa Kenya (CIPK) limesema baadhi ya shule zinawazuia wanafunzi kuhudhuria madrasa kwa kuwaweka shuleni hadi muda wa jioni.

Katibu Mkuu wa CIPK, Mohamed Dor, alisema elimu haipaswi kuangalia ufaulu wa mitihani pekee huku ikipuuza malezi ya kiroho na maadili ya watoto.

Alisema baadhi ya wazazi walilalamika kuwa watoto wao walikuwa wakikosa masomo ya dini wakati wa wiki na hata mwishoni mwa wiki kutokana na ratiba ndefu za shule. Kwa mujibu wake, baadhi ya wanafunzi waliotaka kuhudhuria madrasa walitishiwa hatua za kinidhamu na shule zao.

Kwa mujibu wa kanuni za elimu za Kenya za mwaka 2015, masomo darasani yanapaswa kuanza saa 2 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri, huku michezo na shughuli nyingine zikifanyika baadaye. Hata hivyo, viongozi hao wa Kiislamu wanasema baadhi ya shule zimekuwa zikiongeza vipindi vya ziada kwa lengo la kuongeza ufaulu wa kitaaluma.

Baada ya mazungumzo na viongozi wa CIPK, moja ya shule zilizolalamikiwa ilikubali kuwaachia mapema wanafunzi wanaohudhuria madrasa ili waweze kuendelea na masomo ya dini.

Malalamiko hayo yanakuja miezi kadhaa baada ya serikali ya Kenya kupiga marufuku masomo ya ziada wakati wa likizo ya Disemba kufuatia ongezeko la shule zilizokuwa zikiendelea na vipindi hata baada ya kufungwa rasmi.

Kwa mujibu wa Taifa Leo, Waziri wa Elimu wa Kenya, Julius Ogamba, alisema ni kinyume cha sheria kwa shule kuendesha masomo ya ziada wakati wa likizo na kuahidi hatua kali dhidi ya shule zitakazokaidi maagizo hayo.

Katika kipindi hicho, wazazi na wabunge walilalamikia wanafunzi, wakiwemo watoto wadogo, kulazimishwa kwenda shule mapema sana asubuhi na kubaki kwa muda mrefu kutokana na msisitizo mkubwa wa ufaulu wa mitihani.

## Tanzania nako hali mbaya

Malalamiko kama hayo yamekuwa yakisikika pia Tanzania ambapo shule nyingi zimekuwa zikiendesha masomo ya ziada maarufu kama tuition, hali inayotumia muda ambao watoto wa Kiislamu kwa kawaida wamekuwa wakienda madrasa kusoma masomo ya dini na hivyo kuathiri maendeleo yao ya kiroho.

Mbaya zaidi, masomo hayo ya ziada yamekuwa yakitolewa hata kwa wanafunzi wa shule za msingi — kipindi muhimu zaidi katika ukuaji wa mtoto ambapo anahitaji sana msingi wa elimu ya dini na malezi ya maadili na kiroho.

Kwa upande wa sekondari, baadhi ya wanafunzi huteuliwa kujiunga na shule zilizopo mbali na familia zao, hali inayowafanya kurejea nyumbani wakiwa wamechoka! Ukiongeza masomo ya ziada, hali huwa mbaya zaidi ambapo baadhi ya watoto hurejea majumbani usiku, jambo linalopunguza muda wa familia, mapumziko na elimu ya dini.

Athari za hali hiyo zimekuwa zikionekana wazi kiasi kwamba hata viongozi wa serikali wamekuwa wakieleza wasiwasi kuhusu anguko la maadili miongoni mwa vijana na kuwataka viongozi wa dini kusaidia kurejesha maadili katika jamii.

Katika sherehe za Idd Machi 21, 2026, Samia Suluhu Hassan alizitaka taasisi za dini kusaidia kujenga maadili mema ili kuweka msingi imara wa amani na maendeleo ya taifa, akionya kuwa mmomonyoko wa maadili unaweza kusababisha kukosekana kwa utulivu na kuibuka kwa vurugu.

“Mtetereko wa maadili umetokea ndani ya Taifa letu. Kama wazazi, walezi na viongozi tulitetereka mahali. Turudi tukatizame wapi tulitetereka, tufundishane ili watoto wetu washike maadili,” alisema Rais Samia.

Kwa baadhi ya wadau wa Kiislamu, hali hiyo inaonyesha umuhimu wa kuongeza uwekezaji katika shule za Kiislamu zinazoounganisha elimu ya dini na elimu ya kawaida katika mazingira moja, ili watoto wasilazimike tena kutumia muda mwingi kusafiri kati ya shule na madrasa.

Wengine wanaamini suluhisho ni kuendelea kushinikiza serikali kudhibiti mifumo ya masomo ya ziada inayowaongezea watoto mzigo mkubwa wa masomo huku ikipunguza muda wa malezi ya kiroho na kijamii.



NA ABUU HAYTHAM HASSAN NINGA, MOROGORO

# Aref Nahdi: Wahitimu Forest Hill mkawe mabalozi wa Uislamu

MWENYEKITI wa taasisi ya The Islamic Foundation, Aref Nahdi, amewataka wanafunzi waliohitimu masomo yao katika Shule ya Sekondari ya Forest Hill kuwa mfano bora wa kuigwa katika jamii kwa kuzingatia maadili mema waliyojifunza wakiwa shuleni.

Kauli hiyo imetolewa kwa niaba yake na Mkurugenzi wa Miradi wa taasisi hiyo, Muhammad Aref Nahdi, alipokuwa akizungumza katika mahafali ya kuhitimu kwa wanafunzi wa kidato cha sita wa Shule ya Sekondari ya Forest Hill iliyopo mjini Morogoro na ambayo inamilikiwa na taasisi hiyo.

Akitoa nasaha zake, Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Forest Hill, Ramadhan Sektya, pamoja na mlezi wa taasisi hiyo, mzee Salum Hassan Mdula, waliwataka wahitimu hao kuendelea kudumisha maadili mema, nidhamu na heshima waliyojifunza shuleni hapo ili waweze kuwa viongozi bora wa baadaye.

Naye Katibu wa Idara ya Daawa wa The Islamic Foundation, Sheikh Juma Dhahabau, aliwasisitiza wanafunzi hao kuendelea kushikamana na matendo mema, kumcha Mwenyezi Mungu na kuwa watoto wema kwa wazazi wao pamoja na jamii inayowazunguka.

Awali, Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Onal Dogo, alimkabidhi zawadi maalum Mwenyekiti wa Taasisi ya The Islamic Foundation kwa kutambua mchango wake mkubwa katika maendeleo ya shule hiyo hususan katika sekta ya taaluma na michezo.

Katika Risala ya wanafaunzi hao walitoa pongezi zao kwa uongozi wa Taasisi ya The Islamic Foundation kwa malezi na taaluma bora waliyoipata wakiwa shuleni hapo.



ذُو الحِجّة



# MATUKIO KATIKA PICHA

Na abdulrahman Omar
0655 763 580

## Mahafali ya kuhitimu kwa wanafunzi wa kidato cha sita wa Shule ya Sekondari ya Forest Hill iliyopo mjini Morogoro











HABARI
DAR ES SALAAM

NA MUGINI SINGIRA



# Balozi wa Palestina asimulia madhila wanayopitia

Wapalestina ulimwenguni kote wameadhimisha siku ya Nakba, ikiwa ni kumbukizi ya uvamizi wa Israeli katika ardhi yao ambapo zaidi ya Wapalestina 700,000 walifukuzwa katika makazi yao.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Balozi wa Palestina hapa nchini, Salam Abusharar, amesema Nakba si tukio la zamani pekee bali ni mfumo wa dhuluma unaoendelea hadi leo.

Akitoa simulizi kuhusu kuundwa kwa taifa la Israeli mwaka 1948, Balozi huyo alisema Wapalestina waliwakaribisha wahamiaji wa Kiyahudi waliokuwa wakikimbia mateso barani Ulaya kabla na wakati wa Vita Kuu ya Pili ya Dunia, lakini baadaye walijikuta wakifukuzwa katika ardhi zao wenyewe. "Waliondoka kwenye nyumba zao wakiamini watarudi, lakini waliporudi hawakuruhusiwa tena kuingia kwenye makazi yao," alisema.

Abusharar alieleza kuwa kuundwa kwa taifa la Israel mwaka 1948 kuliambatana na mauaji, uharibifu wa vijiji na kuwafanya maelfu ya Wapalestina kuwa wakimbizi.

Alisema zaidi ya vijiji 530 viliharibiwa huku takriban Wapalestina 750,000 wakiondoshwa kwa nguvu kutoka kwenye makazi yao.

Aidha, alikosoa sheria zilizowekwa baada ya kuundwa kwa Israel, akisema zilitoa nafasi kwa Wayahudi kutoka sehemu mbalimbali duniani kuhamia Israel huku Wapalestina waliopoteza makazi yao wakizuiwa kurejea.

Maadhimisho ya siku ya Nakba mwaka huu yalifanyika Mei 16, 2026 jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na viongozi wa serikali, mabalozi, viongozi wa dini pamoja na wadau mbalimbali wa diplomasia.

ذو الحجة



NA MWANDISHI WETU

# Mwigulu: Rais Samia kufuta sheria ya kutaifisha mali

Waziri Mkuu wa Tanzania, Dk Mwigulu Nchemba amesema Sheria ya Kutaifisha Mali inakwenda kufutwa kwa kuwa, imeshaanza kutumiwa kama kichaka.

Dk Mwigulu alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na wananchi wa Wilaya ya Chemba mkoani Dodoma, eneo la Kambi ya Nyasa ikiwa ni sehemu ya ziara yake ya kikazi.

Msingi wa kusema hayo unatokana na kitendo cha kukamata na kutaifishwa kwa mali na vitendea kazi vya wananachi hali inayokwamisha uzaishaji na utendaji kazi kwa watu waliojiajiri.

“Niwape taarifa njema, Rais ameshaelekeza hiyo Sheria ya Kutaifisha tunakwenda kuifuta, imeshaanza kuwa kichaka na ameshatoa barua nimeipokea inayoelekeza hiyo sheria kufutwa,” alisema.

Wakati akisema hayo, alikuwa ameshikilia nakala za kero za watu zinazoelezea migogoro ya ardhi, watu kunyang’anywa mashamba na mali zao, huku akiendelea kusikiliza migogoro hiyo kutoka kwa wananchi moja kwa moja.

Dk Mwigulu alisema mambo ya kukamata kamata, kushikilia mali na vitendea kazi vya watu, yanapaswa kuachwa kwasababu yanakwamisha juhudi za maendeleo ya kiuchumi.

“Si tu kamata kamata ya wananchi wenyewe hata kukamata vitendea kazi, unakuta jambo linahitaji tu faini nyie mnakamata kitendea kazi. Unakuta kijana anafanya shughuli yake ya bodaboda, baiskeli au gari ndio amefanya kosa, unashikiliaje bodaboda! Imekuwa ya kwenu? Si mnadai faini kama sheria inavyosema?

“Andikisheni kitambulisho chake, andikeni faini yake mwachieni akaendelee na shughuli yake,” alisema.

Alisema kwa watu waliopo serikalini, wanaweza kuwa na uhakika kwa kuwa Serikali haifilisiki, lakini kwa waliojiajiri asipofanya kazi familia nzima inasimama na ukichukua kitendea kazi chake, umeua mtaji na maisha ya familia nzima.

“Unakuta anadaiwa na marejesho, hapa unakuwa umeua na nyumba yake. Niliwahi kwenda Mvumi nikakuta wameshilikia gari ya thamani ya Sh25 milioni kwa deni la Sh700,000 kwa miaka saba.

“Haya mambo ya kukamata kamata na kushikilia vitendea kazi vya watu tuachane nayo. Kama unataka mtu azalishe wewe unakamata kitendea kazi atalipaje?” alihoji.

“Jana nilipita Kondoa nikakuta wamemtuhumu mwizi wamechukua mashine yake ya kusaga hadi kitanda na godoro, sasa wamezoea mimi nimekuja nitawashikisha adabu wote wasio nadabu,” alisema.

Alisema kamata kamata isiyo na msingi ni mambo ya zamani huku akimtaka Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule kuhakikisha anasimamia kulikomesha hilo ili watu waishi wakiwa huru.


Dk Mwigulu alisema ili kupiga hatua kwa kasi kila mmoja anapaswa kuwajibika kuanzia serikalini hadi sekta binafsi ili kila mmoja apate haki yake.

Akizungumzia hilo, Wakili wa kujitegemea, Dk Khamis Masoud kutoka Everlasting Legal Aid Foundation jijini Dar es Salaam, alisema mambo yote ya utaifishwaji yalikuwa katika Azimio la Arusha.

Alisema tatizo sio sheria kufutwa, kwa kuwa Tanzania kunasheria nyingi nzuri, shida inaanzia kwa wasimamizi kuitumia kama fimbo ya kuwachapa wenye haki na wanyonge kwa masilahi yao binafsi.

“Kufuta sheria bado tunaweza kutengeneza tatizo kwa jamii, Serikali inatakiwa kuangalia maadili ya viongozi wake, je inatumika sawa sawa. Mfano mtu ameiba ili kuthibitisha lazima mali zikamatwe zioneshwe; huo ni mchakato wa kisheria na hauna tatizo.

“Inatakiwa tuiboreshe kuhakikisha haitoi mwanya kwa maofisa wenye visa vyao, binafsi wasiitumie vibaya sheria hiyo kuonea watu. Sheria imenyooka ila watu wanavyoitumia ni tatizo.”



MAKALA MAALUM

Na Abeid Othman
0754 990 083

# Tusiigeuze ibada ya hijja kuwa 'outing'



Hijja ni miongoni mwa ibada kubwa kabisa katika Uislamu. Ni nguzo ya tano ambayo Mwenyezi Mungu amewaamrisha Waislamu wenye uwezo kuitekeleza angalau mara moja katika maisha yao. Hii ni safari ya kiroho yenye lengo la kumfanya Muislamu ajikurubishe zaidi kwa Muumba wake, kutubia madhambi, kuimarisha taqwa na kujenga undugu wa Kiislamu baina ya Waislamu kutoka sehemu mbalimbali duniani.

Mwenyezi Mungu amesema katika Qur'an Tukufu: "Na watu wana wajibu kwa Mwenyezi Mungu wa kuhiji kwenye Nyumba hiyo kwa yule awezaye kufunga safari kwenda huko." [3: 97].

Hijja si safari ya starehe bali ni ibada inayohitaji moyo safi, subira, kujinyima na kujiepusha na mambo yanayoweza kuharibu au kupunguza malipo ya ibada hiyo. Ndiyo maana Waislamu wengi hujiandaa kwa muda mrefu kwa kutafuta elimu na kujiweka karibu zaidi na Mwenyezi Mungu kabla ya kwenda Makka,.

## Ni masikitiko makubwa

Hata hivyo, kwa masikitiko makubwa, katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na mwenendo unaotia wasiwasi ambapo baadhi ya watu wameanza kuigeuza ibada ya hijja na hata Umrah kuwa kama sehemu ya kufanya mtoko au "outing". Badala ya kuelekeza muda mwingi katika ibada, dua, dhikri na tafakuri; watu wamekuwa wakitopea kwenye kurekodi video, kupiga picha na kuonesha kila hatua ya safari hiyo kwenye mitandao ya kijamii.

Leo hii, si jambo la kushangaza kumuona mtu akiwa katika eneo takatifu la Msikiti wa Haram, Mina au Arafah lakini akili yake yote ipo kwenye kamera ya simu. Wengine hupiga picha karibu kila hatua ya ibada; wakati wa kutufu, kusai baina ya Safa na Marwah, hata wakati wa dua au ibada za faragha.

Si vibaya mtu kuweka kumbukumbu ya safari yake au kuwafahamisha ndugu zake kuwa amefika salama katika maeneo matukufu. Tatizo linakuja pale ambapo jambo hilo linapozidi kiasi na kuathiri lengo kuu la hijja yenyewe.

Wapo ambao badala ya kujikita katika ibada, huonekana wakitafuta 'angle' maeneo mazuri ya kupiga picha, wakirekodi video za moja kwa moja au kutengeneza maudhui kwa ajili ya mitandao ya kijamii bali hata na hata kujibu maoni. Hii ni hatari kubwa kwa sababu inaweza kuondoa unyenyekevu na khushuu unaotakiwa katika ibada hiyo adhimu.

Ni muhimu kuelewa kuwa hijja ni safari ya kujisafisha kiroho. Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) amesema kuwa mwenye kuhiji kwa Ikhlasi na akajiepusha na mambo maovu hurudi akiwa msafi wa madhambi kama siku aliyozaliwa na mama yake. Fadhila hii kubwa haiwezi kupatikana kwa urahisi ikiwa moyo wa mtu umejawa na kujionyesha au kushughulishwa zaidi na mambo ya dunia.

Katika Uislamu, kuna maasi yanaitwa riya, yaani kufanya ibada kwa lengo la kuonekana au kusifiwa na watu. Hili ni kosa kubwa kwa mujibu wa Sharia ya Kiislamu. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alionya sana kuhusu riya kwa sababu huharibu amali njema. Mtu anaweza kutumia fedha nyingi, akapoteza muda wake lakini nia yake ikichanganyika na kutafuta mbele za watu, thawabu zake zinaweza kupungua au hata kutoweka kabisa.

Kwa kuiona hatari hii wanazuoni wa Kiislamu wamekuwa wakisisitiza umuhimu wa Ikhlasi katika ibada zote, hasa hijja. Yabidi mtu ajitenge na mambo yanayomtoa katika utulivu wa kiroho. Simu za mkononi na mitandao ya kijamii ni miongoni mwa vitu vinavyoweza kuvuruga ibada ikiwa havitatumiwa kwa kiasi na hekima.

Nisisitize tena Makka na Madina si maeneo ya starehe za kidunia bali ni ardhi tukufu anbako dua hujibiwa, machozi ya toba humwagika na rehema za Mwenyezi Mungu hushuka kwa wingi. Mahujaji wanatakiwa kutumia kila dakika vizuri kwa ajili ya ibada na si kwa mambo yasiyo na ulazima.

## Tutunze adabu za hijja

Ni muhimu masheikh na waandaaji wa safari za hijja kuendelea kutoa elimu kwa mahujaji kuhusu adabu za hijja na namna bora ya kuitunza ibada hiyo dhidi ya mambo yanayoweza kuipunguzia thamani. Elimu itolewe kabla ya safari na hata wakati wa ibada yenyewe.

Aidha, familia na jamii kwa ujumla zinapaswa kuacha tabia ya kuwapa presha mahujaji kutuma picha kila wakati au kufanya matangazo ya kila hatua ya safari yao. Wakati mwingine mazingira haya hupelekea watu wajione wanalazimika kuonesha kila wanachokifanya huko Makka na Madina.

Hakuna ubaya kwa mtu kuweka kumbukumbu chache za safari yake ya hijja. Lakini jambo hilo lifanyike kwa kiasi, kwa adabu na bila kuathiri ibada yenyewe. Lengo kuu la hija si kuonekana wala kupata umaarufu katika mitandao ya kijamii, bali ni kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu.

NA MWANDISHI WETU

# UN yaitaja Tanzania ya tatu katika kuvutia watalii



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dkt. Ashatu Kijaji, amesema Tanzania imefanikiwa kuwa miongoni mwa vinara duniani kwa kuvutia watalii wengi wa kimataifa.

Dkt. Kijaji amesema hayo bungeni jijini Dodoma wakati akiwasilisha makadirio ya bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Alisema ongezeko hilo limefikia asilimia 7.1 kwa mujibu wa mizania ya dunia iliyofanywa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Utalii (UN Tourism). Kwa rekodi hizo, UN Tourism imeitaja Tanzania kuwa ya tatu duniani kwa soko la utalii lililofanya vizuri.

Akielezea mafanikio hayo, Dkt. Kijaji alisema idadi ya watalii ilifikia zaidi ya milioni 5.9 mwaka 2025, ikiwa ni ongezeko la asilimia 10.7 ikilinganishwa na watalii milioni 5.3 mwaka 2024.

Aidha, Dkt. Kijaji amempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa mchango wake mkubwa katika kuitangaza sekta ya utalii kimataifa, hususan kupitia filamu za Tanzania: The Royal Tour na Amazing Tanzania, hatua ambayo amesema imeongeza idadi ya watalii nchini.

# Mfumo mpya wa viwango EAC kuleta ahueni kwa wafanyabiashara

Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC) imeitisha kikao cha Kamati ya Viwango ya jumuiya hiyo kwa ajili ya kujadili mkakati wa kikanda wa kulinganisha mifumo ya ubora.

Hatua hiyo inalenga kutatua changamoto ya mizigo inayopimwa katika mipaka ya nchi moja kukubalika katika nchi nyingine bila mfanyabiashara kulazimika kupima tena.

Kamati hiyo ya viwango inatarajiwa kupitisha viwango vipya takribani 90 vitakavyopelekwa ngazi ya juu kwa ajili ya kutangazwa katika Gazeti la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Mkurugenzi wa Uandaaji Viwango wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TBS), David Ndibalema, amesema hayo katika mkutano wa 28 wa Kamati ya Viwango ya EAC uliofanyika Mei 13, 2026 jijini Arusha.

Ndibalema amesema hadi sasa idadi ya viwango vilivyolinganishwa ndani ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki imefikia takribani 2,163.

Akifafanua malengo ya majadiliano hayo, amesema yanakusudia kuwezesha biashara, kupunguza vikwazo visivyo vya kikodi na kurahisisha usafirishaji wa huduma pamoja na bidhaa ndani ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Mkutano huo wa Kamati ya Viwango umewakutanisha nchi wanachama, kamati ndogo za kitaalamu, washirika wa maendeleo pamoja na taasisi za kitaifa na kimataifa zinazojihusisha na uandaaji na ulinganishaji wa viwango. Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Mapato Kenya, Esther Ngari, amesema kamati ndogo zilizokutana zimejadili kwa kina uoanishaji wa viwango ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

“Viwango hivi vitatusaidia kufanya biashara kati ya nchi na nchi mara tu tutakapooanisha viwango hivyo. Hivi sasa tunapitia na kujadili ripoti za mwaka pamoja na mipango kazi ya kamati ndogo kwa mwaka 2026/2027,” aliongeza kusema.




HABARI

NA MWANDISHI WETU

DAR ES SALAAM

# Waliofadhiliwa Hijja na Rais Museveni wawasili Madina

Mahujaji 150 waliofadhiliwa na serikali ya Uganda chini ya Rais Yoweri Museveni wamewasili salama mjini Madina, wakielekea kuanza ibada na ziara katika Msikiti wa Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) kabla ya kuelekea Makka kutekeleza nguzo ya tano ya Uislamu.

Safari hiyo iliyoongozwa na Imam Ahmad Sulaiman Kyeyune imefanyika katika makundi matatu katika safari zilizofanyika kuanzia Mei 10 hadi 17.

Ujumbe huo unasimamiwa na msaidizi maalum wa rais anayeshughulikia habari na uhamasishaji, Haji Faruk Kirunda. Kwa mujibu wa taarifa kutoka Ikulu ya Uganda, kila Hijja imegharimu dola 5,500 za Marekani, sawa na zaidi ya shilingi milioni 14 za Uganda kwa kila muumini.


Wakati huo huo, kampuni ya Tawakal Travels nchini Uganda imewaaga zaidi ya mahujaji 60 wanaotarajiwa kuelekea Makka na Madina kwa ibada ya Hijja ya mwaka 2026 chini ya kampeni ya Salam Road to Makkah inayolenga kusaidia Waislamu wa Uganda kutekeleza ibada hiyo.

Kwa mujibu wa Nile Post, katika hafla iliyofanyika katika Msikiti wa Magoba, viongozi wa dini waliwataka mahujaji hao kutumia vizuri muda wao katika ibada, kudumisha nidhamu na kuliombea taifa lao wakiwa katika ardhi takatifu.

Taarifa mbalimbali zinaonesha kuwa zaidi ya Waislamu milioni 1.5 kutoka mataifa tofauti wanatarajiwa kushiriki Hijja ya mwaka 2026 nchini Saudi Arabia, jambo linaloifanya kuwa moja ya mikusanyiko mikubwa zaidi ya kidini duniani. Hatua ya Rais Museveni imeongeza taswira ya mshikamano wa kitaifa na kuimarisha ushirikiano kati ya serikali na Waislamu nchini Uganda, ambao ni takribani asilimia 14 ya wananchi wote kwa mujibu wa takwimu za sensa ya taifa hilo

Hatua hiyo pia imepokelewa vyema katika duru za Kiislamu Afrika Mashariki, huku baadhi ya viongozi wa dini wakisema ufadhili huo ni ishara ya kuthamini mchango wa Waislamu katika maendeleo ya taifa. Mahujaji hao wanatarajiwa kurejea Uganda baada ya kukamilisha ibada za Hijja katika miji mitakatifu ya Makka na Madina.

# Mufti Uganda ahimiza utoaji wa zaka, asifu udhamini wa mahujaji



Katika hali iliyoonyesha umuhimu wa mshikamano na kuwajali wenye uhitaji, Mufti wa Uganda, Shaban Ramadhan Mubaje, ametoa wito mzito kwa Waislamu kote nchini kuongeza juhudi katika utoaji wa zaka na misaada kwa jamii, akisisitiza kuwa kutoa si kupunguza mali bali ni njia ya kuleta baraka na kuilinda dhidi ya hasara zisizotarajiwa.

Akizungumza katika hafla ya kuwaaga mahujaji iliyofanyika mjini Tororo, Mufti Mubaje alisema kuwa moja ya nguzo muhimu za mafundisho ya Kiislamu ni kuwasaidia wenye mahitaji na kuhakikisha kuwa neema ambazo Mwenyezi Mungu amewajaalia baadhi ya watu zinakuwa daraja la kuinua maisha ya wengine. Kwa mujibu wa taarifa zilizoripotiwa na Nile Post, kiongozi huyo wa kidini alieleza kuwa jamii yenye watu wanaojitoa kusaidia wengine huwa na mshikamano wa kudumu na hupunguza changamoto zinazotokana na umasikini na kukosekana kwa matumaini.

Mufti Mubaje alisisitiza kuwa mali ambayo haijaambatana na baraka haiwezi kudumu kwa muda mrefu, akiongeza kuwa Waislamu wanapaswa kuelewa kuwa zaka ni wajibu wa kidini unaolenga kusafisha mali na kuimarisha ustawi wa jamii kwa ujumla. Alisema mara nyingi watu hujihusisha zaidi na kutafuta mali bila kufikiria namna ya kuigawa kwa haki kwa wale walioko katika mazingira magumu.

Katika hafla hiyo, Mufti huyo alimpongeza mfanyabiashara mashuhuri Abdullahi Hussein Shire kwa kitendo chake cha kugharamia safari ya Hajj kwa Waislamu wanane mwaka huu. Alisema hatua hiyo ni mfano bora wa kuigwa na wafanyabiashara wengine wenye uwezo, kwani inaonesha namna utajiri unavyoweza kutumika kuleta mabadiliko chanya katika maisha ya watu na kuimarisha ibada.

Mbali na hilo, Mufti Mubaje aliwataka wazazi kuweka mkazo katika malezi ya watoto kwa kuhakikisha wanapata elimu ya dini sambamba na elimu ya kawaida.

ذُو الحِجَّة



NA MWANDISHI WETU

# Ubabe wa Mazayuni kuvamia Al-Aqsa waibua hasira duniani

Mvutano mpya umeibuka katika Msikiti wa Al-Aqsa mjini Jerusalem Mashariki baada ya mawaziri wa mrengo mkali wa serikali ya Israel kuvamia eneo hilo huku maelfu ya Wazayuni wakifanya maandamano yaliyosheheni kauli za chuki dhidi ya Wapalestina.

Kwa mujibu wa ABC News Australia, maelfu ya Wazayuni walikusanyika katika Mji Mkongwe wa Jerusalem kuadhimisha kumbukumbu ya vita vya mwaka 1967 ambapo Israel ilichukua udhibiti wa Jerusalem Mashariki.

Ripoti hiyo ilieleza kuwa baadhi ya washiriki wa maandamano hayo walikuwa wakipaza kauli kama "Waarabu wafe" na "Palestina ifutwe," hali iliyowalazimu wafanyabiashara wengi wa Kipalestina kufunga maduka yao kwa hofu ya mashambulizi na uharibifu.

Wakati huo huo, Waziri wa Usalama wa Taifa wa Israel, Itamar Ben-Gvir, aliingia katika eneo la Msikiti wa Al-Aqsa akiwa chini ya ulinzi mkali wa polisi na kupeperusha bendera ya Israel, hatua iliyozusha ukosoaji mkubwa duniani.

Kwa mujibu wa Anadolu Agency, Saudi Arabia ililaani hatua hiyo ikiitaja kama uchokozi unaokiuka hadhi ya kihistoria na kisheria ya maeneo matakatifu ya Jerusalem.

Shirika la Ushirikiano wa Kiislamu (OIC) nalo lilisema ziara hiyo ni "shambulio la wazi" dhidi ya Waislamu duniani. OIC via QNA

Misri, Jordan, Qatar na Uturuki pia zimetoa matamko ya kulaani hatua hiyo, zikionya kuwa vitendo hivyo vinaweza kuongeza mvutano katika eneo hilo ambalo tayari linakabiliwa na vita vya Gaza na hali mbaya ya kibinadamu. Egypt Today Jordan Times Qatar MFA

Wachambuzi wanaonya kuwa kuongezeka kwa matukio kama hayo katika Al-Aqsa kunaweza kuongeza zaidi hasira na kutishia juhudi za kurejesha utulivu katika eneo la Mashariki ya Kati.



ذو الحجة

**HABARI**
**DAR ES SALAAM**

NA YUSUPH AMIN

# Maandalizi ya Hijja Saudi Arabia yapamba moto



Serikali ya Saudi Arabia imeongeza maandalizi makubwa ya msimu wa Hijja kwa kuboresha huduma, miundombinu na teknolojia katika maeneo matakatifu ya Mina, huku ikisisitiza usalama na ustawi wa mamilioni ya mahujaji wanaotarajiwa kuwasili mwaka huu.

Naibu Gavana wa Makkah, Prince Saud bin Mishaal, amefanya ziara maalum kukagua maendeleo ya miradi inayolenga kuhudumia mahujaji watakaotekeleza nguzo ya tano ya Uislamu.

Kwa mujibu wa taarifa rasmi, zaidi ya kambi 54,000 zimeandaliwa Mina pamoja na vituo karibu 200 vya huduma na matengenezo, huku maeneo ya malazi yakienea katika zaidi ya mita za mraba milioni 3.5. Serikali pia imejenga njia zenye vivuli zaidi ya mita za mraba 100,000 ili kupunguza athari za joto kali kwa mahujaji.

Aidha, zaidi ya feni 400 za kunyunyizia ukungu wa maji pamoja na ngazi za umeme 74 zimewekwa katika eneo la Jamarat ili kusaidia kupunguza msongamano wa watu wakati wa ibada.

Wakati huo huo, Saudi Arabia imezindua teknolojia mpya ya kupima uimara wa barabara zinazotumiwa wakati wa Hijja kupitia kifaa kinachoitwa Heavy Traffic Load Simulator, hatua inayotajwa kuwa ya kwanza ya aina yake katika Mashariki ya Kati.

Kwa mujibu wa Saudi Gazette, kifaa hicho kina uwezo wa kufanya mizunguko 26,000 ya majaribio ndani ya saa 24 ili kuiga msongamano mkubwa wa magari unaotokea wakati wa Hijja kwa zaidi ya miaka 20 ijayo.

Teknolojia hiyo pia inaweza kupima ubora wa lami katika mazingira ya joto na baridi kati ya nyuzi 15 hadi 60 za sentigredi, hatua inayolenga kuongeza uimara wa barabara, kupunguza gharama za matengenezo na kuimarisha usalama wa mahujaji.

Wizara ya Afya ya Saudi Arabia pia imetangaza chanjo ya homa ya uti wa mgongo kuwa lazima kwa wafanyakazi wote wa Hijja mwaka huu, sambamba na kuhimiza chanjo za mafua ya msimu na UVIKO-19.

Uwekezaji huo mkubwa unaonyesha namna Saudi Arabia inavyoendelea kutumia teknolojia, miundombinu na huduma za kisasa kuboresha mazingira ya Hijja kila mwaka, hasa wakati idadi ya mahujaji duniani ikiendelea kuongezeka baada ya kurejea kwa safari za kawaida kufuatia miaka ya janga la corona.

Hijja ya mwaka huu inatarajiwa kuwakutanisha zaidi ya Waislamu milioni 1.5 kutoka mataifa mbalimbali duniani.

***Chanzo: Muslim Networks, Saudi***




UKHTI FATIMA SS

# KAZANFORUM 2026: Dunia ilivyokongamana Urusi kwa uwekezaji halal

Kongamano la kimataifa la Russia–Islamic World: KazanForum 2026 limehitimishwa mjini Kazan nchini Urusi huku likiweka rekodi mpya ya ushiriki wa mataifa na kuimarisha nafasi yake kama jukwaa muhimu la ushirikiano wa kiuchumi kati ya Urusi na ulimwengu wa Kiislamu.

Kongamano hilo la siku sita lililofanyika kuanzia Mei 12 hadi 17 katika Jamhuri ya Tatarstan, lilikutanisha zaidi ya washiriki 10,000 kutoka mataifa 103, huku mijadala mikubwa ikijikita katika biashara ya halal, fedha za Kiislamu, usalama wa chakula, viwanda, teknolojia na uwekezaji wa kimataifa.

Rais wa Tatarstan, Rustam Minnikhanov, alisema sekta ya halal inaendelea kukua kwa kasi duniani huku Tatarstan ikijitokeza kama moja ya vituo muhimu vya uchumi wa halal nchini Urusi.

Alisema mauzo ya nje ya bidhaa za halal kutoka Tatarstan yalifikia dola milioni 45 mwaka jana, kiwango kilichoongezeka mara tatu ikilinganishwa na mwaka uliopita, huku zaidi ya wazalishaji 150 wa bidhaa za halal wakifanya kazi katika eneo hilo.

Katika kongamano hilo, viongozi na wataalamu wa uchumi walisisitiza kuwa halal sasa si suala la chakula pekee bali mfumo mpana wa biashara unaohusisha maadili, fedha, utalii, huduma na uwekezaji wa kimataifa.

Katibu Mkuu wa Islamic Chamber of Commerce and Development, Youssef Hassan Khalawi, alisema halal ni falsafa ya biashara inayoweka mbele maadili na uaminifu katika mahusiano ya kiuchumi.

Fedha za Kiislamu nazo zilijitokeza kama moja ya ajenda kuu za kongamano hilo huku wataalamu wakisema mfumo huo unaweza kuwa chanzo muhimu cha fedha kwa ajili ya miradi ya miundombinu na maendeleo ya viwanda katika Urusi na nchi za CIS.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya AAOIFI kutoka Bahrain, Sheikh Ibrahim bin Khalifa Al-Khalifa, alisema hamasa ya fedha za Kiislamu katika Urusi na mataifa ya CIS imeongezeka kwa kiasi kikubwa katika mwaka uliopita huku Tatarstan ikitajwa kuwa miongoni mwa maeneo yanayoongoza katika kukuza benki za Kiislamu kupitia mifumo ya elimu na udhibiti.

## Wawekezaji Ghuba wasisimua sekta fedha za Kiislamu Asia ya Kati

**Sekta ya fedha za Kiislamu inaendelea kukua kwa kasi katika nchi za Asia ya Kati huku uwekezaji kutoka mataifa ya Ghuba na maboresho ya sheria yakitajwa kuchochea maendeleo hayo. Kwa mujibu wa ripoti ya Arab News, serikali za nchi kama Kazakhstan, Uzbekistan, Kyrgyzstan na Azerbaijan zimeanza kufanya mageuzi ya kisheria ili kuimarisha huduma za benki za Kiislamu, sukuk na takaful.**

**Shirika la Islamic Development Bank (IsDB) limetoa zaidi ya dola bilioni 10 kwa nchi za eneo hilo hadi Aprili mwaka huu, huku Uzbekistan, Kazakhstan na Kyrgyzstan zikinufaika zaidi.**

**Mkuu wa fedha za Kiislamu wa taasisi ya Fitch Ratings, Bashar Al-Natoor, alisema sekta hiyo bado ipo katika hatua za awali lakini kasi ya ukuaji inaongezeka kutokana na ushiriki wa wawekezaji kutoka mataifa ya Ghuba.**

**Ripoti hiyo ilieleza kuwa idadi kubwa ya Waislamu, kiwango kikubwa cha watu wasiokuwa na huduma rasmi za benki na ongezeko la mahitaji ya bidhaa zinazofuata misingi ya Shariah vinaifanya Asia ya Kati kuwa soko muhimu la baadaye kwa fedha za Kiislamu.**

## Wasiokuwa Waislamu wakubali ubora, usafi bidhaa halal

**Sekta ya chakula cha halal duniani inaendelea kukua kwa kasi huku ongezeko la idadi ya Waislamu, mahitaji ya vyakula salama na mwelekeo wa matumizi ya bidhaa zenye maadili vikichochea ukuaji huo.**

**Kwa mujibu wa Vocal Media, soko la chakula cha halal linatarajiwa kuongezeka kutoka dola trilioni 2.89 mwaka 2025 hadi dola trilioni 6.39 ifikapo mwaka 2034.**

**Ripoti hiyo, ikinukuu taasisi ya Renub Research, ilieleza kuwa sekta hiyo itakuwa ikikua kwa wastani wa asilimia 9.14 kwa mwaka kati ya 2026 na 2034. Mbali na Waislamu, ripoti hiyo ilisema hata wasiokuwa Waislamu wanaongezeka kutumia bidhaa za halal kutokana na kuamini kuwa zina viwango bora vya usafi, ufuatiliaji wa bidhaa na uzalishaji wenye kuzingatia maadili. Idadi ya Waislamu duniani pia inatajwa kuwa kichocheo kikubwa cha ukuaji huo. Ripoti inaonyesha kuwa idadi hiyo inaweza kufikia watu bilioni 2.8 ifikapo mwaka 2050, sawa na karibu asilimia 30 ya watu wote duniani.**

**Sekta ya nyama ya halal inaendelea kuongoza soko hilo, huku bidhaa zilizosindikwa, pipi, vitafunwa na vyakula vya haraka nazo zikionyesha ukuaji mkubwa.**

**Wataalamu wanasema ukuaji huo unaifanya halal kuwa si soko la kidini pekee tena, bali moja ya sekta kubwa zaidi katika uchumi wa chakula duniani.**

## Brazil yaanza kuvutia soko la utalii wa halal

**Brazil imeanza kuongeza juhudi za kuvutia watalii Waislamu kupitia mafunzo maalum kuhusu huduma za halal yaliyotolewa katika maonesho ya utalii ya Tourism Expo yaliyofanyika Fortaleza, kaskazini mashariki mwa nchi hiyo.**

**Kwa mujibu wa ANBA News, Chama cha Biashara kati ya Waarabu na Brazil (ABCC) kilitoa warsha kuhusu "Utalii na Ukarimu kwa Soko la Halal," kikieleza fursa za biashara zinazohusiana na watalii Waislamu.**

**Meneja wa miradi ya kimataifa wa ABCC, Fernanda Dantas, alisema uchumi wa halal ni miongoni mwa sekta zinazokua kwa kasi zaidi duniani na unatarajiwa kufikia thamani ya dola trilioni 10.8 ifikapo mwaka 2027.**

**Ripoti iliyowasilishwa katika maonesho hayo ilionyesha kuwa utalii wa halal pekee unatarajiwa kuzalisha dola bilioni 384 duniani.**

ذو الحجة

Na Abeid Othman
0754 990 083

# Tukithirishe kusambaza elimu ya mifumo ya kifedha ya Kiislamu

Katika zama hizi za maendeleo ya uchumi na upanuzi wa huduma za kifedha duniani, suala la elimu kuhusu mifumo ya kifedha ya Kiislamu limekuwa muhimu sana kuliko wakati mwingine wowote.

Kwa bahati mbaya, bado Waislamu wengi hawana maarifa ya kutosha kuhusu mfumo wa fedha wa Kiislamu na huduma za kibenki zinazofuata misingi ya Sharia. Upungufu huu wa elimu umesababisha wengi kuamini kuwa benki za Kiislamu hazina tofauti kubwa na benki za kawaida zinazotumia riba.

Matokeo yake, sehemu kubwa ya Waislamu wamekuwa wakizikwepa huduma hizi na kubaki kwenye mifumo inayowaweka katika nafasi kubwa ya kwenda kinyume na dini yao.

Uislamu umeweka mfumo kamili wa maisha unaogusa nyanja zote za mwanadamu, ikiwemo uchumi na fedha. Mfumo wa kifedha wa Kiislamu umejengwa juu ya misingi ya uadilifu, uwazi, kugawana faida na hasara, pamoja na kuzuia dhuluma.

Moja ya mambo yaliyokatazwa wazi katika Uislamu ni riba. Allah Mtukuka ameharamisha riba kwa sababu inaleta ukandamizaji na kuathiri usawa wa kijamii.

Hata hivyo, Waislamu wengi hawajui kuwa mfumo wa kifedha wa Kiislamu umeandaliwa mahsusi kutoa mbadala halali wa huduma za kifedha bila kutumia riba.

## Shida iko hapa

Tatizo kubwa lililopo ni ukosefu wa elimu na mawaidha ya kutosha kutoka kwa viongozi wa dini, taasisi za Kiislamu na wadau wa uchumi wa Kiislamu.

Watu wengi wanaingia benki za Kiislamu bila kuelewa misingi yake. Wengine husikia tu majina kama "Murabaha", "Mudaraba", "Ijara" au "Musharaka" lakini hawaelewi maana yake.

Kutokana na kutoelewa huku, baadhi yao hudhani kuwa benki za Kiislamu zimebadilisha majina tu lakini huduma zake ni sawa na za benki za riba. Dhana hii imeenea sana katika jamii na imekuwa sababu ya wengi kukataa kushiriki katika huduma za kifedha za Kiislamu.

Ni muhimu kuelewa kuwa benki za Kiislamu zinafanya kazi kwa misingi tofauti kabisa na benki za kawaida. Katika benki za kawaida, fedha hutolewa kwa mkopo wenye riba ambayo lazima irejeshwe bila kujali hali ya biashara au maisha ya mkopaji. Kwa upande wa mfumo wa Kiislamu, benki hushiriki kwenye biashara au uwekezaji kwa misingi ya kugawana faida na hasara.

Mfumo huu unaweka haki kwa pande zote na kuondoa unyonyaji. Aidha, fedha katika mfumo wa Kiislamu lazima zitumike katika shughuli halali zinazokubalika kisharia.

Kutokana na ukosefu wa elimu, Waislamu wengi wameendelea kukimbilia huduma za kifedha zenye riba huku wakidhani hakuna njia mbadala. Hili ni jambo la kusikitisha kwa sababu kwa sasa dunia imepiga hatua kubwa katika maendeleo ya uchumi wa Kiislamu.

## Hatuna udhuru

Leo hii kuna huduma nyingi za kifedha zinazofuata Sharia ambazo zinaweza kuwasaidia Waislamu kuendesha maisha yao bila kuingia katika riba.

Miongoni mwa huduma hizo ni sukuk, takaful, mifuko ya uwekezaji wa Kiislamu, pamoja na benki za Kiislamu zinazotoa huduma mbalimbali za biashara na uwekezaji.

Sukuk ni moja ya fursa kubwa katika mfumo wa kifedha wa Kiislamu. Hizi ni hati fungani zinazofuata misingi ya Sharia tofauti na hati za kawaida zinazotegemea riba.



Kupitia sukuk, wawekezaji hushiriki katika miradi halali na hupata faida kutokana na mafanikio ya mradi husika. Mfumo huu unahamasisha uwekezaji wenye tija na unaojenga uchumi wa jamii.

Vilevile, takaful ni mfumo wa bima ya Kiislamu unaojengwa juu ya kusaidiana na kuchangiana katika majanga.

Tofauti na bima za kawaida ambazo mara nyingi huhusishwa na riba na gharar, takaful huzingatia misingi ya ushirikiano na uwazi.

Mfumo huu unatoa kinga ya kifedha kwa washiriki bila kuvunja sheria za Kiislamu. Hata hivyo, bado Waislamu wengi hawajui umuhimu wake wala namna unavyofanya kazi. Kutokana na hali hii, kuna haja kubwa ya kuimarisha elimu na mawaidha kuhusu mifumo ya kifedha ya Kiislamu. Masheikh, maimamu na walimu wa dini wanapaswa kufanya kazi kubwa ya kuelimisha jamii kuhusu uchumi wa Kiislamu.

Mimbari za misikiti, madrasa, vyombo vya habari na mitandao ya kijamii vitumike kueneza maarifa haya muhimu. Elimu hii isibaki kwa wataalamu wa benki pekee, bali iwafikie Waislamu wa kawaida ili waweze kufanya uamuzi sahihi katika maisha yao ya kifedha.

Aidha, taasisi za Kiislamu zinapaswa kuandaa semina, makongamano na vipindi vya elimu vitakavyofafanua tofauti kati ya benki za Kiislamu na benki za riba.

Wataalamu wa uchumi wa Kiislamu washirikiane na viongozi wa dini ili kutoa elimu iliyo wazi na yenye kueleweka kwa jamii.

Ikiwa juhudi hizi zitafanyika kwa nguvu kubwa, Waislamu wengi wataondokana na dhana potofu kuwa huduma za kifedha za Kiislamu ni sawa na zile za kawaida.

Faida ya kuwa na elimu ya kutosha kuhusu mifumo ya kifedha ya Kiislamu ni kubwa sana. Kwanza, itasaidia Waislamu kujiepusha na riba ambayo imeharamishwa katika dini. Pili, itaimarisha uchumi wa Kiislamu kwa sababu watu wengi wataanza kutumia huduma zinazofuata Sharia

Tatu, itajenga jamii yenye uadilifu na usawa wa kiuchumi kwa sababu mfumo wa Kiislamu unazingatia haki kwa kila mshiriki.

NA UKHTI FATIMA



# Fedha zinaweza kukupeleka mbali na Allah – au karibu zaidi Naye

**Kuna baadhi ya Waislamu wanaoamini kuwa kujihusisha sana na fedha, biashara au uwekezaji ni jambo linaloweza kumweka mtu mbali na dini. Mara nyingi utasikia kauli kama: "Mimi sitaki dunia sana," "Fedha zinaharibu watu," au "Muhimu ni dini, si utajiri."**

**Kwa nje, kauli hizi zinaweza kuonekana za kiroho na zenye unyenyekevu. Lakini wakati mwingine zinaweza kuficha uelewa usio kamili kuhusu nafasi ya mali ndani ya Uislamu.**

Tatizo si fedha. Tatizo ni namna fedha zinavyopatikana na kutumika.

Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) alisema: "Muumini mwenye nguvu ni bora na anapendwa zaidi na Allah kuliko muumini dhaifu." Wanazuoni wengi wameeleza kuwa nguvu hapa haihusishi mwili pekee, bali pia uwezo wa kiuchumi, akili na uthabiti wa maisha.

Muislamu maskini anayeshindwa kulipa ada za watoto, kugharamia matibabu, kusaidia wazazi au kutoa sadaka huwa katika mazingira magumu zaidi ya utegemezi na udhaifu wa kijamii.

Fedha zenye baraka zinaweza kuwa kinga dhidi ya fedheha, madeni, utegemezi na hata maovu.

Ndiyo maana Qur'an haikukataza mali. Badala yake, ilikataza mali inayopatikana kwa dhulma, riba na njia haramu. Qur'an pia imejaa maelekezo kuhusu biashara, mirathi, zaka, matumizi ya mali na kusaidia jamii. Hii inaonyesha kuwa Uislamu haukuja kuondoa mali, bali kuisafisha.

## Mali inaweza kuwa ibada

Wapo wanaosema: "Fedha zinamuweka mtu mbali na Pepo."

Lakini Qur'an inasema: "Mfano wa wanaotoa mali zao katika njia ya Allah ni kama punje iliyoota masuke saba, katika kila suke kuna punje mia." [Qur'an 2:261]. Hii ina maana kuwa mali inaweza kuwa njia ya kukupeleka karibu zaidi na Allah ikiwa itatumika vizuri.

Kwa fedha, unaweza kujenga kisima, kusaidia yatima, kufadhili elimu ya Kiislamu, kujenga msikiti, kusaidia dawah au kuwasaidia ndugu wenye shida. Hayo yote yanaweza kuendelea kukuandikia thawabu hata baada ya kufa.

Kwa hiyo, tatizo si kuwa na fedha. Tatizo ni fedha kukumiliki badala ya wewe kuimiliki.

## Hauko salama eti kwa kutokujishughulisha tu

Wengine hujifariji wakisema: "Mimi sifanyi haramu yoyote ikiwa siweki fedha kwenye uwekezaji."

Lakini katika mfumo wa kisasa wa uchumi, kutofanya chochote si mara zote jambo lisilo na madhara. Fedha zilizowekwa benki, mifuko ya hifadhi au uwekezaji zinaweza kutumika kufadhili riba, pombe, kamari au biashara nyingine ambazo Muislamu asingependa kuzihusisha na mali yake.

Qur'an inaonya kuhusu riba kwa lugha kali sana: "Msipoacha riba, basi pokeeni tangazo la vita kutoka kwa Allah na Mtume wake." (Qur'an 2:279)

Ndiyo maana mjadala wa uwekezaji wa halal si mjadala wa "anasa za kidunia" pekee. Ni mjadala wa uwajibikaji wa mali.

Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) anasema: "Yeyote miongoni mwenu atayeona jambo ovu na baya basi aliondoshe kwa mkono wake, ikiwa hawezi kuliondoa kwa mkono wake basi aliondoe kwa ulimi wake, na ikiwa hawezi kuliondoa kwa ulimi basi na alichukie kutoka moyoni mwake, na kuchukia moyoni ni udhaifu wa imani." [Muslim].

## Hutachukua fedha kaburini — lakini...

Baadhi ya watu husema: "Sitachukua utajiri wangu kaburini."

Ni kweli. Akaunti za benki zitabaki duniani. Lakini namna ulivyotafuta na kutumia mali yako haitabaki duniani.

Mtume Muhammad (rehema na amani zimshukie) alisema kuwa mwanadamu ataulizwa Siku ya Kiyama kuhusu mali yake — alipataje na aliitumiaje.

Hilo ndilo suala kubwa zaidi.

Uislamu haumfundishi Muislamu kuukimbia ulimwengu kabisa. Unamfundisha kuutumia ulimwengu bila kuupoteza Akhera. Maswahaba wengi wakubwa walikuwa wafanyabiashara na watu wenye uwezo mkubwa wa kifedha, lakini mali haikuingia mioyoni mwao kuliko Allah.

## Tatizo si fedha — ni uelewa wetu kuhusu fedha

Katika dunia ya leo, Muislamu anahitaji si tu ibada nzuri, bali pia ufahamu mzuri wa fedha, uwekezaji wa halal na namna ya kutumia mali kwa njia yenye baraka.

Fedha zinaweza kukutoa kwenye dini ikiwa zitakuwa chanzo cha kiburi, tamaa, dhulma au kusahau Akhera.

Lakini fedha zinaweza pia kuwa daraja la sadaka, hifadhi ya familia, msaada kwa jamii na uwekezaji wa Akhera.

Mwisho wa siku, swali si kama una fedha nyingi au chache.

Swali ni: fedha zako zinakupeleka wapi?

MAHMOUD NYAMGUMA

# Saudi Arabia yashinikiza mkataba wa kutoshambuliana na Iran



Saudi Arabia inaongoza juhudi za kutaka mataifa ya Ghuba na Iran kuingia makubaliano ya kutoshambuliana ili kupunguza mvutano wa kisiasa na kijeshi katika Mashariki ya Kati kufuatia vita vya hivi karibuni kati ya Iran na muungano wa Marekani na Israel.

Kwa mujibu wa The New Arab na Greater Kashmir, mpango huo unaungwa mkono na baadhi ya mataifa ya Ulaya pamoja na taasisi za Umoja wa Ulaya.

Ripoti hizo zilisema Saudi Arabia inatazama mfano wa makubaliano ya Helsinki ya mwaka 1975 yaliyosaidia kupunguza mvutano kati ya mataifa ya Magharibi na Umoja wa Kisovieti wakati wa Vita Baridi.

Mataifa ya Ghuba yana hofu kuwa Iran, licha ya kudhoofishwa na vita vya hivi karibuni, inaweza kuendelea kuwa tishio kutokana na uwezo wake wa makombora na ndege zisizo na rubani (drones). Hata hivyo, baadhi ya wanadiplomasia wanaona kuwa makubaliano hayo yanaweza kuwa magumu kufanikiwa bila kuwepo kwa maelewano kati ya Iran na Israel, huku tofauti za kisiasa kati ya Saudi Arabia na Falme za Kiarabu (UAE) nazo zikitajwa kuwa changamoto nyingine.

## Uhaba wa oksijeni watishia maisha ya maelfu Gaza

**Uhaba mkubwa wa oksijeni katika hospitali za Gaza umeendelea kuhatarisha maisha ya maelfu ya wagonjwa huku mashambulizi na uharibifu wa miundombinu ya afya vikizidisha hali mbaya ya kibinadamu katika eneo hilo.**

**Kwa mujibu wa Al Khabar Al Yemeni, Wizara ya Afya Gaza imesema vituo 22 kati ya 34 vya uzalishaji wa oksijeni vilivyokuwa vikihudumia hospitali vimeharibiwa, huku vilivyosalia vikifanya kazi kwa kusuasua kutokana na ukosefu wa vipuri.**

**Ripoti hiyo ilieleza kuwa wagonjwa wengi wanaolazimika kutumia oksijeni wanakabiliwa na hatari kubwa ya kupoteza maisha endapo huduma hiyo itakatika hata kwa muda mfupi.**

**Mgonjwa mmoja mwenye umri wa miaka 60, Alaa al-Harani, alisema kuchelewa kwa oksijeni kwa hata chini ya saa moja kunaweza kusababisha kifo chake kutokana na hali mbaya ya kiafya anayopitia.**

## Mfalme Salman atuzwa kwa miaka 60 ya kuunga mkono hifdh ya Qur'an

**Mfalme wa Saudi Arabia, Salman bin Abdulaziz Al Saud, ametunukiwa heshima maalum kwa mchango wake wa zaidi ya miaka 60 katika kusaidia vyama na taasisi za kuhifadhi Qur'an nchini humo.**

**Kwa mujibu wa Saudi Gazette, zawadi hizo zilipokelewa kwa niaba yake na Mwanamfalme na Waziri Mkuu Mohammed bin Salman wakati wa hafla maalum iliyofanyika Jeddah.**

**Miongoni mwa zawadi hizo kulikuwa na ngao ya heshima, nakala ya Qur'an iliyoandikwa kwa mkono pamoja na bango lililoonyesha kuwa Mfalme Salman alikamilisha kuhifadhi Qur'an akiwa na umri wa miaka 10. Bango jingine lilikuwa na majina ya zaidi ya wahifadhi wa Qur'an 21,000 walionufaika kupitia Jumuiya ya Kuhifadhi Qur'an ya Riyadh (Maknoon).**

**Taarifa hiyo ilieleza kuwa heshima hiyo ni kutambua mchango wa Mfalme Salman katika kuendeleza ufundishaji wa Qur'an, tafsiri zake, elimu za Qur'an pamoja na kusambaza tafsiri za Qur'an katika lugha mbalimbali duniani.**

## Wanafunzi Waislamu karibu nusu ya wanafunzi wote Vienna

**Idadi ya wanafunzi Waislamu katika shule za umma jijini Vienna, nchini Austria imefikia asilimia 42 huku baadhi ya shule za kati na taasisi za ufundi zikikaribia asilimia 49, kwa mujibu wa takwimu zilizochapishwa Mei 2026 na gazeti la Die Presse. Takwimu zinaonesha wanafunzi Wakatoliki ni 17% pekee kati ya wanafunzi zaidi ya 114,000 waliopo katika mfumo wa elimu wa jiji hilo. Ukuaji huo unaelezwa kuchochewa na ongezeko la familia za Kiislamu kutoka Uturuki, Mashariki ya Kati na maeneo mengine ya Ulaya.**

**Ongezeko hilo linaashiria kuimarika kwa jamii ya Kiislamu barani Ulaya katika kipindi ambacho makanisa mengi yakikabiliwa na kupungua kwa Waumini. Ripoti mbalimbali zinaonyesha**

## KUTOKA KWA MHARIRI

ذو الحجة

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
+255 789 201383

# Tutumie vyema siku 10 Tukufu za Dhul-Hijja

Tumesisitizwa kuzidisha matendo mema katika siku kumi za mwanzo wa Dhul–Hijja, kwani ndizo siku bora na tukufu zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu kuliko siku nyingine zote za mwaka.

Ubora wa siku hizi umetajwa katika Qur'an Tukufu pale Mwenyezi Mungu aliposema: "Naapa kwa Alfajiri. Na naapa kwa siku kumi." [Qur'an, 89:1–2]. Wanazuoni wa tafsiri ya Qur'an wamekubaliana kuwa siku kumi zilizokusudiwa katika aya hii ni siku kumi za mwanzo wa Dhul–Hijja.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu awafanyie wepesi Waislamu wote waliokwenda kutekeleza ibada ya Hijja mwaka huu. Na sisi tuliosalia nyumbani, tumuombe Mwenyezi Mungu atuwezeshe kuzifikia fadhila za siku hizi kumi za mwanzo wa Dhul–Hijja.

Hizi ni siku muhimu kwa Waislamu kushindana katika kujikusanyia thawabu alizotuahidi Mwenyezi Mungu, huku tukiamini kuwa mwenye kufanikiwa ni yule atakayezitumia vyema siku hizi kwa kufanya mambo mengi ya kheri.

### Siku 10 zenye baraka

Mwanazuoni Ibn Kathir (Allah amrehemu) amesema: "Muradi wa siku kumi zilizotajwa katika Suratul–Fajr ni siku za mwanzo za mwezi wa Dhul–Hijja." Kauli hiyo pia imenukuliwa kutoka kwa Ibn Abbas, Ibn Zubeir na Mujahid.

Katika hadith iliyosimuliwa na Ibn Abbas (Allah amuwie radhi), Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Hakuna siku ambazo amali njema zinapendwa zaidi na Mwenyezi Mungu kuliko siku hizi", yaani siku kumi za mwanzo wa Dhul–Hijja.

Masahaba wakauliza: "Ewe mjumbe wa Allah, je hata kuliko Jihad katika njia ya Allah?" Mtume akajibu: "Hata Jihad katika njia ya Allah, isipokuwa mtu aliyetoka mwenyewe na mali yake kwenda kupigana Jihad, kisha asirudi na chochote katika hivyo." [Bukhari].

Pia Mtume amesema katika hadith nyingine: "Hakuna siku tukufu zaidi ambazo amali zinapendeza zaidi mbele ya Allah kuliko siku hizi kumi. Basi kithirisheni Tahlil, Takbira na Tahmid." [Twabarani].

Kutokana na hadith hizi mbili, tunajifunza kuwa siku kumi za kwanza za mwezi wa Dhul–Hijja ni tukufu sana na ni fursa adhimu kutoka kwa Allah kwa waja wake wema. Hivyo, haifai kwa Muislamu kuzembea au kutozipa uzito siku hizi.

Jambo jingine la kuzingatia ni kuwa fursa hii haikutolewa kwa mahujaji pekee, bali ni kwa Waislamu wote. Hivyo, hata wewe uliyebaki katika mji wako unaweza kuitumia fursa hii kwa njia mbalimbali.



### Yanayopendekezwa kufanywa

Miongoni mwa mambo yanayopendekezwa ni kuswali sala zote kwa jamaa pamoja na kuzidisha sala za Sunna za usiku na mchana (Nawaafil). Sala ndiyo nguzo ya ibada zote, na mwenye kuitekeleza ipasavyo huwa amejikurubisha kwa Allah Ta'ala.

Ushahidi wa hilo ni kisa cha Sahaba Thawban (Allah amridhie), ambaye alimuomba Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amuombee dua ili awe pamoja naye Peponi. Mtume alimwambia: "Jilazimishe kusujudu kwa wingi (kusali sana), kwani hutosujudu sijda moja kwa ajili ya Allah isipokuwa itakusogeza hatua moja karibu naye na kukufutia kosa moja." [Muslim].

Kadhalika, kufunga swaumu za Sunna, hususan siku ya Arafa ni katika mambo muhimu mno. Muislamu akifunga siku moja tu kwa ajili ya Allah huwekwa mbali na Moto umbali wa mwendo wa miaka 70.

Funga inapotekelezwa katika siku hizi tukufu malipo yake ni makubwa mno. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alipoulizwa kuhusu funga ya siku ya Arafa alisema: "Nataraji kwa funga hii Allah atafuta madhambi ya mwaka uliopita na ya mwaka ujao." [Muslim].

Aidha, tumesisitizwa kujipamba na sifa ya ukarimu kwa kuwasaidia masikini, mafukara na wasiojiweza kwa lengo la kutafuta radhi za Allah, si kwa kujionesha. Jambo hili limehimizwa ili kudhihirisha ushirikiano wa kweli wa kiroho katika utekelezaji wa maagizo ya Allah hapa duniani.

### Kufanya toba ya kweli

Wanazuoni wametubainishia kuwa ni muhimu kwa mja katika siku hizi tukufu kukumbuka makosa na madhambi aliyoyatanguliza, kisha kumuomba Allah msamaha. Vilevile, mja atumie siku hizi kuwaomba radhi wale aliowakosea. Hili ni jambo la msingi katika kufikia hatua ya kukubaliwa matendo.

SHEIKH Shaaban Mussa
0786 272 323

# Umoja wa Kiislamu, matunda ya Ramadhan katika jamii

Miongoni mwa mafundisho makubwa na yenye athari ya moja kwa moja kwa jamii ambayo Ramadhan huyaimarisha ni umoja na mshikamano wa Waislamu. Ndani ya mwezi huo mtukufu, Waislamu kutoka matabaka yote —matajiri na maskini, viongozi na wananchi wa kawaida— hukusanyika katika ibada moja, kwa wakati mmoja, na kwa lengo moja: kumwabudu Mwenyezi Mungu.

Hali hii huonesha kwa uwazi kwamba Uislamu ni dini ya umoja na si ya mgawanyiko. Waislamu huamka pamoja kwa ajili ya daku, hufunga pamoja mchana, na hufuturu pamoja jioni. Pia huswali pamoja misikitini, husikiliza Qur'an pamoja, na hushiriki ibada za usiku kwa moyo mmoja.

Mwenyezi Mungu anasisitiza umuhimu wa umoja kwa kusema: "Na shikamaneni kwa Kamba ya Mwenyezi Mungu nyote pamoja, wala msifarikiane..." [Qur'an, 3: 103]. Aya hii inaweka msingi mkubwa wa maisha ya Kiislamu: kwamba nguvu ya Umma ipo katika kushikamana kwake.

Aidha, Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Muumini kwa Muumini mwenzake ni kama jengo; sehemu moja huimarisha nyingine." [Bukhari na Muslim]

Katika Ramadhan, hadith hii huonekana kwa vitendo. Watu hushindana kulisha wenye kufunga, kusaidia wahitaji, kutoa sadaka, na kuwafariji waliodhoofika. Misikiti hujaa watu wa aina mbalimbali, lakini wote husimama safu moja bila ubaguzi wa cheo, rangi, au mali. Hapo ndipo Uislamu huonesha uzuri wake wa kweli.

Ule mshikamano wa Ramadhan hujenga hisia ya udugu wa kweli baina ya Waislamu. Tajiri hujihisi karibu na maskini, mwenye nguvu humhurumia dhaifu, na kila mmoja hujifunza kwamba wote ni sawa mbele ya Mwenyezi Mungu. Hakuna anayekuwa bora isipokuwa kwa taqwa na matendo mema.

Lakini swali muhimu ni hili: je, umoja huu huendelea baada ya Ramadhan kuisha?

Kwa bahati mbaya, baada ya Ramadhan baadhi ya jamii za Waislamu hurudi katika tofauti, migawanyiko, na wakati mwingine uhasama. Mshikamano uliokuwa umejengwa katika mwezi mtukufu hupungua, na kila mtu huanza kujishughulisha na mambo yake binafsi.

Hii huonesha kwamba somo la umoja halikueleweka kikamilifu au halikuhifadhiwa ipasavyo. Kwa sababu Ramadhan haikuja kutuunganisha kwa mwezi mmoja tu, bali kutufundisha namna ya kuishi pamoja kwa amani maisha yote.



Historia ya Kiislamu pia inathibitisha kuwa umoja ni siri ya mafanikio ya Umma. Waislamu waliposhikamana katika nyakati za mwanzo wa Uislamu, waliweza kujenga jamii yenye elimu, haki, na ustaarabu mkubwa. Lakini kila waliporuhusu fitina na migawanyiko kuingia, walidhoofika na kupoteza nguvu yao.

Umoja wa Kiislamu ni msingi muhimu wa nguvu ya Umma. Pale Waislamu wanapokuwa na mshikamano, huweza kushinda changamoto nyingi za kijamii, kiuchumi, na hata kiimani. Lakini wanapogawanyika, hupoteza nguvu na heshima yao.

Miongoni mwa njia za kudumisha umoja baada ya Ramadhan ni kuendelea kushiriki pamoja katika ibada za kijamii kama vile swala za jamaa misikitini, vikao vya elimu, na shughuli za kusaidiana. Haya yote huimarisha uhusiano baina ya Waislamu na huondoa hisia za ubinafsi.

Aidha, ni muhimu kujifunza kuvumiliana katika tofauti ndogo ndogo. Waislamu wanaweza kuwa na mitazamo tofauti katika baadhi ya masuala ya kifiqhi au kijamii, lakini hilo halipaswi kuwa sababu ya kugombana au kutengana. Tofauti zisipodhibitiwa kwa hekima hugeuka kuwa chanzo cha chuki na migawanyiko.

Imam Shafi (Allah amrehemu) aliwahi kusema: "Maoni yangu ni sahihi lakini yanaweza kuwa na makosa, na maoni ya mwingine ni makosa lakini yanaweza kuwa sahihi." Haya ni mafunzo makubwa ya ustaarabu wa tofauti ndani ya Uislamu.

Pia, kusaidiana katika shida na raha ni nguzo muhimu ya umoja. Muislamu anapaswa kumjali ndugu yake kama anavyojijali mwenyewe. Mtume amesema: "Hatokuwa ameamini mmoja wenu mpaka ampendelee ndugu yake anachokipenda nafsi yake." [Bukhari na Muslim].

Hii hujenga jamii yenye upendo, huruma, na mshikamano wa kweli.

Ramadhan pia hutufundisha kwamba umoja haujengwi kwa maneno tu, bali kwa vitendo. Kushirikiana katika ibada, kusaidiana katika matatizo, kutembeleana, kusameheana, na kushikamana katika maisha ya kila siku ndiyo msingi wa kuimarisha udugu wa Kiislamu.

Kwa hakika, jamii ya Waislamu yenye umoja ni jamii yenye baraka na nguvu. Na jamii iliyogawanyika ni dhaifu hata kama ina rasilimali nyingi.

Hivyo basi, baada ya Ramadhan, kila Muislamu anapaswa kujiuliza: je, ninachangia kuimarisha umoja au kuuvunja? Je, ninamwona ndugu yangu wa Kiislamu kama mshirika wangu au kama mpinzani wangu? Je, maneno na matendo yangu yanajenga upendo au yanaeneza chuki?

Kwa sababu Umma wenye kushikamana hupendwa na Mwenyezi Mungu, hupewa nguvu, na huishi kwa utulivu na heshima.

Lakini pamoja na umoja wa jamii, kuna jambo jingine muhimu sana ambalo Ramadhan hulilenga kwa kiwango kikubwa, nalo ni kujenga tabia ya kuirekebisha nafsi (muhasaba na toba ya kudumu).

Katika makala inayofuata, tutazungumzia kuhusu Toba na Kujirekebisha – Safari Endelevu Baada ya Ramadhan, na jinsi ya kuifanya toba kuwa sehemu ya maisha ya kila siku.

ذوالحِجة فتاوى



**SHEIKH**
**Shaaban Mussa**
**0786 272 323**

# Nini fadhila za siku 10 za Dhul-Hijjah?

**Swali:** **Tunaomba kubainishiwa yaliyopokelewa kuhusu ubora wa siku kumi za Dhul-Hijjah, na je, kuna ibada maalumu zinazopendekezwa katika siku hizi?**

**Jibu:** Kuhusu fadhila za siku kumi za Dhul-Hijjah na ibada zinazopendekezwa, ndani yake kuna maelezo yenye kutosha na baraka.

## Fadhila za Siku Kumi za Dhul-Hijjah:

Katika hadith iliyopokewa na Imam Bukhari na wengineo na kusimuliwa na Ibn Abbas (Allah amridhie Yeye na baba yake), Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Hakuna siku ambazo matendo mema hupendwa zaidi na Mwenyezi Mungu ndani yake kuliko siku hizi kumi."

Swahaba wakauliza: "Hata Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu?" Akasema: "Hata jihad katika njia ya Mwenyezi Mungu, isipokuwa mtu aliyetoka na nafsi yake na mali yake kisha hakurudi na chochote."

Naye Imam Ahmad akipokea kutoka kwa Ibn Umar (Allah amridhie Yeye na baba yake) akieleza kuwa Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Hakuna siku zilizo kubwa zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu wala zinazopendwa zaidi kwake kwa matendo kuliko siku hizi kumi, basi zikithirisheni ndani yake tahlili (Laa ilaaha illa Allah), takbiri na tahmid."

Na Ibn Hibban amepokea kutoka kwa Jabir (Allah amridhie) kwamba Mtume amesema: "Hakuna siku iliyo bora zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu kuliko Siku ya Arafa."

## Aina za ibada katika siku hizi

### Mosi, kuhiji na kufanya Umrah

Hii ndiyo ibada bora zaidi inayoweza kufanywa katika siku hizi. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Umrah moja hadi nyingine ni kafara ya dhambi zilizo baina yake, na Hijja iliyokubaliwa haina malipo isipokuwa Pepo."

### Pili, kufunga

Kwa wasiokuwa mahujaji, imependekezwa kufunga siku hizi au baadhi yake, hasa Siku ya Arafa. Katika Hadith Qudsi Mwenyezi Mungu amesema: "Funga ni kwa ajili Yangu, na Mimi ndiye nitakayelipa ujira wake."

Na Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Hakuna mja anayefunga siku moja katika njia ya Mwenyezi Mungu isipokuwa Mwenyezi Mungu humuepusha uso wake na Moto kwa umbali wa miaka sabini."

Pia amesema Mtume kuhusu siku ya Arafa: "Ninatarajia kwa Mwenyezi Mungu kwamba kufunga Siku ya Arafa kutafuta dhambi ya mwaka uliopita na mwaka unaofuata."

### Tatu, Takbiri na kumtaja Mwenyezi Mungu kwa wingi

Mwenyezi Mungu amesema: "Na walitaje jina la Mwenyezi Mungu katika siku maalumu." [Qur'an, 22:28]. Wanazuoni wamefafanua kuwa siku hizo ni siku kumi za Dhul-Hijjah.

Miongoni mwa dhikri zinazopendekezwa ni Takbiri, Tahlili, Tahmidi na Tasbihi. Mfano wa takbiri ni kusema: "Allahu Akbar, Allahu Akbar, Laa ilaaha illa Allah, Allahu Akbar, Allahu Akbar wa Lillahil Hamd." Kadhalika, inapendekezwa kuinua sauti kwa takbiri katika masoko, nyumba, misikiti na njia mbalimbali.

### Nne, kutubu na kuacha maasi

Ni muhimu kutumia siku hizi kwa kutubia dhambi, kuacha maasi na kurejea kwa Mwenyezi Mungu kwa Ikhlas. Ikumbukwe kuwa maasi husababisha mtu kuwa mbali na rehema za Mwenyezi Mungu, na utiifu huleta ukaribu na mapenzi yake.

### Tano, kuzidisha matendo mema

Matendo mema ni pamoja na swala za sunna, sadaka, kusoma Qur'an, kuwasaidia watu na kuamrisha mema pamoja na kukataza maovu. Matendo haya mema, kwa ujumla, katika siku hizo yana ujira mkubwa sana.

### Sita, takbiri Mutlaq na Muqayyad

Takbiri Mutlaq ni takbiri inayosemwa wakati wowote mchana, usiku, nyumbani, njiani na hata msikitini kuanzia mwanzo wa Dhul-Hijjah hadi mwisho wa siku za Tashriq. Kwa upande wa pili, Takbiri Muqayyad huletwa tu baada ya swala za faradhi. Takbiri hii kwa wasiokuwa mahujaji huanza Alfajiri ya Siku ya Arafah ilhali kwa kwa mahujaji huanza baada ya Adhuhuri ya Siku ya Idd. Takbiri hizi huendelea hadi Alasiri ya mwisho wa siku za Tashriq.

### Saba, kuchinja Udh-hiya (Qurbani)

Hii ni sunna kubwa ya Nabii Ibrahim na Mtume Muhammad (Allah awashushie rehema na amani). Imepokewa kwamba Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alichinja kondoo wawili wenye pembe, akasema Bismillah na Takbiri wakati wa kuchinja.



NA YUSUFU AMINI

# Jipime kama una yakini ya kweli kwa Allah

Ipo dhana iliyojengeka katika jamii kuwa kifo ndiyo mwisho wa maisha ya binadamu. Dhana hiyo imejengwa na uzoefu wa kila siku ambapo watu huzaliwa, huishi na hatimaye hufa.

Kauli kama, "Hakuna Pepo wala Moto, nani alikwenda akarudi?" zimekuwa zikitolewa na baadhi ya watu, wakiwamo Waislamu, kwa mtazamo wa kutaka ushahidi wa moja kwa moja kuhusu maisha baada ya kifo.

Katika mtazamo wa Uislamu, imani juu ya uwepo wa Pepo, Moto na maisha baada ya kifo hupatikana kupitia ufunuo (wahyi) na mafundisho ya dini. Kwa hiyo, Muislamu wa kweli huamini kuwepo kwa Pepo, Moto na maisha baada ya kifo kwa msingi wa wahyi kutoka kwa Allah na ujumbe wa Mitume wake (amani iwashukie wote).

Hata kama hakuna aliyekufa kisha akarejea duniani kutoa simulizi ya moja kwa moja kama wanavyotaka baadhi ya watu, hoja ya dini hubaki kuwa si kila jambo linathibitishwa kwa kuona.

Kuna mambo mengi ambayo watu huyakubali kupitia ushahidi wa kiakili, hisia, taarifa za kuaminika au athari zake. Kwa msingi huo, Muislamu anatakiwa kuwa na jambo moja muhimu litakalompa nguvu ya kuendelea kusimama imara, nalo ni yakini kwa Allah.

Yakini ni imani isiyo na chembe ya shaka katika kumwamini Allah kwa kila jambo. Mwenye yakini hupata utulivu hata anapokumbana na matatizo, kwa kuwa moyo wake umefungamana na Mola wake Mlezi.


Yakini ndiyo iliyowafanya Mitume wa Allah wavumilie majaribu makubwa na kusimama imara bila kuyumba. Allah ameeleza umuhimu wa yakini katika Qur'an Tukufu aliposema: "Na katika ardhi zipo ishara kwa wenye yakini." [Qur'an, 51:20].

Aya hii inaonesha kuwa mtu mwenye yakini huona alama za uwepo na uwezo wa Allah katika kila jambo linalomzunguka. Anaangalia mbingu, ardhi, maisha na mauti, kisha imani yake huimarika.

Miongoni mwa yakini kubwa anayopaswa kuwa nayo Muislamu kila siku ni kuamini kuwa Allah ndiye msimamizi wa maisha yake. Watu wengi huishi kwa hofu ya kesho; wengine huogopa kukosa kazi, riziki au msaada wa watu.

Ama muumini wa kweli huamini kuwa riziki yake iko kwa Allah. "Na hakuna kiumbe chochote kitembeacho ardhini isipokuwa riziki yake iko kwa Allah..." [Qur'an, 11:6].

Yakini hii humfanya Muislamu kufanya kazi kwa bidii huku akijiepusha na haramu. Haibi, hadhulumu wala kukata tamaa kwa sababu anajua alichopangiwa na Allah hakiwezi kuchukuliwa na mwingine. Anajitahidi kufanya kazi huku moyo wake ukimtegemea Allah pekee.



Yakini humfundisha muumini kuwa Allah humjibu mja wake kwa wakati bora zaidi, na kamwe hamdhulumu. Licha ya ukweli huo, wapo baadhi yetu wanaokata tamaa baada ya kumuomba Allah kwa muda mrefu bila kuona majibu ya haraka.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesisitiza umuhimu wa kuwa na yakini katika dua aliposema: "Muombeni Allah hali ya kuwa mna yakini ya kujibiwa." [Tirmidhi].

Hadith inatufundisha kuwa dua si maneno ya kawaida, bali ni ibada inayopaswa kutoka katika moyo wenye imani kamili kwa Allah. Muislamu anatakiwa kumuomba Allah huku akiwa na matumaini makubwa ya kujibiwa.

Suala jingine muhimu ni kuamini kuwa kila jambo linalotokea lina hekima ndani yake hata kama huioni kwa wakati huo. Wakati mwingine mtu huachishwa kazi, biashara hushuka au hupatwa na maradhi na kuiona dunia imemtupa.

Muumini mwenye yakini huamini kuwa nyuma ya kila mtihani kuna kheri. Huenda kile unachokiona leo kuwa hasara kikawa sababu ya kupata neema kubwa kesho.

Allah anatuambia: "Huenda mkachukia jambo nalo lina kheri kwenu. Na huenda mkapenda jambo nalo lina shari kwenu. Na Mwenyezi Mungu anajua na nyinyi hamjui." [Qur'an, 2:216]. Katika aya hii, Allah anawapa faraja wale wanaopitia changamoto mbalimbali maishani.

Aidha Mtume amesema: "...hakika (muumini) mambo yake yote ni kheri. Akipata neema hushukuru, nayo huwa kheri kwake; na akipatwa na dhiki husubiri, nayo huwa kheri kwake." [Sahih Muslim].

Hii ndiyo tofauti kati ya moyo wenye yakini na moyo usio na yakini. Mtu asiye na yakini hufadhaika haraka anapopatwa na matatizo, lakini mwenye yakini huendelea kuwa na matumaini hata katika mazingira magumu.

Katika zama hizi ambazo watu wengi wanapitia sonona, msongo wa mawazo na kukata tamaa, kurejea kwa Allah ni jambo muhimu sana. Yakini kwa Allah humfanya mtu kupata utulivu wa moyo, ambao hauwezi kununuliwa kwa mali wala kupatikana kwa umaarufu.

MAKALA MAALUM

SHEIKH Seif Ruga
0712 690 811



# Misingi ya hukumu katika ndoa ya Kiislamu

**Mkataba wa ndoa ni miongoni mwa mikataba iliyopewa umuhimu mkubwa katika Uislamu kutokana na utukufu na upekee wake, kwani unahusiana na heshima za watu, nasaba na kuendelea kwa kizazi cha binadamu. Ikumbukwe kuwa athari za ndoa haziishii kwa mwanamke peke yake, bali zinavuka hadi kwa familia na jamii kwa ujumla.**

Kutokana na umuhimu huo, wanazuoni wengi wameweka sharti la kuwepo kwa msimamizi (walii) katika mkataba wa kufunga ndoa kwa sababu ya maslahi mbalimbali yaliyomo ndani yake. Wapo wanaoona kuwa walii ni nguzo ya kusihi kwa ndoa, hivyo ndoa haifungwi bila ridhaa yake, huku wengine wakiona kuwa si nguzo na kwamba ndoa inaweza kufungwa kwa kauli ya mwanamke mwenyewe.

Hata hivyo, walii anatakiwa kumuomba ridhaa mwanamke na kumshauri, na wala hana haki ya kumzuia au kumdhuru.

Miongoni mwa ufafanuzi mzuri zaidi wa maana ya msimamizi katika mkataba wa ndoa (walii) ni ule wa Awadh al–Awfi aliyesema: "(Walii) ni mamlaka ya kisharia kwa jamaa wa nasaba wa upande wa baba au wanaochukua nafasi yao, kwa ajili ya kumuozesha yule ambaye hastahiki kufunga ndoa mwenyewe."

Usimamizi wa mkataba wa ndoa (wilaya) umegawanyika katika aina mbili; usimamizi wa ulazimashaji (Ijbaar) na usimamizi wa hiari (uchaguzi). Usimamizi wa ulazimashaji ni ule ambao walii ana mamlaka ya kufunga ndoa bila kuomba idhini ya mtu aliye chini ya huduma na ulinzi wake.

Wanazuoni wametofautiana mitazamo kuhusu nani anayekuwa na mamlaka ya usimamizi huu. Kwa mujibu wa madhehebu ya Kishafi, baba mzazi na babu mzaa baba pekee ndio wenye mamlaka ya kumlazimisha mwanamke bikira asiyeweza kupambanua maslahi katika mkataba wa ndoa.

Usimamizi wa hiari ni pale mwanamke anaposhirikiana na walii wake katika kuchagua mume, na walii hana haki ya kumlazimisha. Jukumu lake ni kusimamia mkataba wa ndoa baada ya mwanamke huyo kuposwa na mwanaume anayemridhia.

Huu ni mtazamo wa Jopo la Wanazuoni wa madhehebu matatu ya Malik, Hanbali na Shafi. Usimamizi huu wa ndoa ya hiari husimamiwa na mawalii wengine tofauti na wasimamizi wa kulazimisha.

Kwa upande wa madhehebu ya Hanafi, wanaona kuwa mwanamke mwenye akili timamu na aliyebalehe, awe bikira au aliyeolewa kabla, ana haki ya kujifungisha ndoa. Hata hivyo, inapendekezwa kwake kumkabidhi walii wake jukumu hilo kwa heshima na adabu.

Hoja ya Jopo la Wanazuoni kuhusu kutosihi kwa mkataba wa ndoa bila kuwepo walii ni kauli ya Allah Mtukufu isemayo: "Na mtakapowataliki wanawake wakafikia muda wa kumaliza eda yao, msiwazuie kuolewa na waume zao (wa awali) ikiwa wameridhiana baina yao kwa mujibu wa ada..." [Qur'an, 2:232].



Aya hii tukufu inakataza mawalii kuwazuia wanawake baada ya kumaliza eda zao ikiwa wanataka kurejea kwa waume wao wa zamani kupitia ndoa mpya. Hili ndilo andiko lililo wazi zaidi katika Qur'an, kwamba walii hana haki ya kumzuia mwanamke ikiwa ameridhia kuolewa kwa njia iliyo ya kheri.

Kwa upande wao, wanazuoni wa madhehebu ya Hanafi wanaona kuwa mwanamke mwenye akili timamu na aliyebalehe anaweza kufunga ndoa yake mwenyewe na hata ya mwingine, ingawa jambo hilo si bora na linakwenda kinyume na utaratibu wa ndoa.

Mtazamo huo unatokana na kauli ya Ibn Abbas (Allah amridhie) kwamba, Mtume wa Allah (rehama na amani ziwe juu yake) amesema: "Mwanamke asiye na mume (ayyim) ana haki zaidi juu ya nafsi yake kuliko msimamizi (walii) wake, na bikira huombwa idhini yake kuhusu nafsi yake, na idhini yake ni kunyamaza kwake."

Kinachoonekana kutokana na maandiko ya pande zote mbili ni kwamba, rai ya Jopo la Wanazuoni ndiyo iliyo sahihi zaidi kutokana na nguvu ya uthibitisho na maandiko waliyoyajengea hoja.

Msimamizi wa mkataba wa ndoa (walii) ana masharti yanayopaswa kutimia ili awe na sifa ya kuwa walii. Baadhi ya masharti hayo yamekubaliwa na wanazuoni wote, huku mengine wakitofautiana mitazamo.

Masharti yaliyokubaliwa na wote ni walii kuwa Muislamu, balehe na mwenye akili timamu, pia awe na uwezo wa kupambanua mambo (rushd). Masharti waliyotofautiana ni uadilifu, pamoja na kutokuwa katika utekelezaji wa ibada ya Hijja au Umra.

Mawalii katika ndoa ya mwanamke wa Kiislamu ni jamaa wa upande wa baba (asaba). Wanazuoni wa madhehebu nne wametofautiana mitazamo kuhusu mpangilio wa nani anayetangulizwa kuliko mwingine.

Kwa upande wa madhehebu ya Shafi, anayestahiki zaidi kumuozesha mwanamke ni baba, kisha babu wa upande wa baba na kuendelea kupanda juu kinasaba, kisha ndugu wa tumbo moja, kisha ndugu wa baba, na baadaye watoto wao kwa kushuka chini kinasaba.

MAKALA MAALUM SEHEMU YA 2

Na Said Rajab
0783 650 803




# Hajra, alama ya uongozi na ujenzi wa jamii

**Tulieleza katika makala iliyopita kwamba, Allah 'Azza Wajallah' alimuongoza Nabii Ibrahim kumuacha Hajra na mwanawe katika nchi kame. Kupitia kujitolea, uvumilivu, ustahimilivu, mahangaiko na imani yake kwa Mwenyezi Mungu, Hajra alithibitisha kwamba wanawake wana uwezo wa kujenga jamii bora. Leo tumalizie sehemu ya mwisho kwa kumulika nafasi ya mama Hajra katika kuunda maadili na ustaarabu wa jamii yake.**

Kimsingi, mwanamke akipewa fursa anaweza kuunda ustaarabu mzima yeye peke yake. Nabii Ibrahim (amani ya Allah imshukie) alijua kwamba nafasi kama hiyo ya uongozi haiwezi kuoneshwa katika jamii iliyotawaliwa na mfumo dume kwa karne nyingi, jamii ambayo haina heshima kubwa kwa wanawake.

Hata hivyo, kupitia mama Hajra, Mwenyezi Mungu anatuonesha nguvu, uadilifu, na uthabiti wa mwanamke katika kutimiza jukumu hilo zito. Suala hapa ni kubomoa ubaguzi wa kijinsia na dhana kwamba mwanamke hawezi kuchukua jukumu muhimu katika maisha ya jamii.

Uzoefu wa mama Hajra kwenye nchi kame ulikuwa wa thamani sana kiasi kwamba Mwenyezi Mungu ameuhifadhi katika taratibu zinazohusiana na ibada ya Hijja.

Kwa mahujaji, matendo ya kunywa maji ya Zamzam, kuzunguka Al–Ka'aba, kukaa Mina na kulala Muzdalifa, kukimbia baina ya Safa na Marwa – milima ambayo Mwenyezi Mungu ameitaja kuwa ni mitakatifu – pamoja na kuchinja wanyama, yote hayo yanahusishwa na mama Hajra na mwanawe Ismail.

Ndugu zangu katika imani, Hajra si mwanamke wa kawaida katika historia ya imani ya Mungu Mmoja asiye na mshirika. Uongozi wake ulijenga njia ya umoja huko Makka miongoni mwa waumini wanaotoka sehemu mbalimbali za dunia.

Mwenyezi Mungu ameihifadhi taasisi ya Hijja ili kuwakumbusha watu kwamba Yeye ni Mmoja asiye na mshirika, na kwamba wanadamu wote wana asili moja, na pia wanawake wanaweza kuwa viongozi kwa maana halisi ya neno hilo.

Hajra ndiye mwanamke pekee katika historia kuunda ustaarabu wa watu wanaomuabudu Mungu Mmoja, ambapo pia alibomoa dhana potofu ya ubaguzi wa kijinsia. Alionesha kwamba hata katika upweke na mazingira hatarishi zaidi, mwanamke anaweza kulinda heshima na hadhi yake na kuonesha uongozi madhubuti bila kuyumba hata kidogo.

Alithibitisha kwamba uongozi unatokana na kujitoa kwa dhati katika kusimamia fikra sahihi na hauna uhusiano wowote na migawanyiko ya kijinsia. Isitoshe, aliweka msingi kwamba wanawake pia wana nafasi muhimu katika kutafuta ustawi wa jamii na kwamba jambo hilo siyo la wanaume peke yao.

Wanaume na wanawake, kila mmoja ana jukumu sawa na mwingine kulingana na maumbile yao. Mama Hajra alithibitisha kwamba mwanamke anaweza kuwa na mtazamo chanya hata katika mazingira magumu na hatari kiasi gani iwapo atamtegemea Mwenyezi Mungu.

Mama Hajra alikuwa hivyo kwa sababu Allah alimpa heshima kwa kuweka uongozi wake katika mfumo wa ibada ya Hijja.

***Itaendelea wiki ijayo, Insha Allah***

MAKALA MAALUM

Na Junaynat Ally Dama
0789 201 383

# Misingi minne ya mafanikioya kimkakati

Katika dunia ya leo yenye ushindani mkubwa, kufanya kazi kwa juhudi pekee haitoshi tena. Taasisi, biashara na hata watu binafsi wanahitaji uwezo wa kufikiri na kutenda kimkakati (strategically) ili kufikia mafanikio ya muda mrefu.

Wataalamu wa uongozi na biashara wanaeleza kuwa mafanikio mengi ya kudumu hujengwa juu ya misingi minne muhimu: fikra za kimkakati, mwelekeo wa kimkakati, mipango ya kimkakati na utekelezaji wa kimkakati.

## Fikra za kimkakati (Strategic thinking)

Msingi wa kwanza ni uwezo wa kufikiri zaidi ya matatizo ya muda mfupi.

Watu wenye fikra za kimkakati hawaangalii tu kilicho mbele yao leo, bali pia matokeo ya baadaye ya maamuzi wanayofanya sasa. Wao hujiuliza: "Je, tunafikiria kwa upana wa kutosha?"

Wataalamu wanasema fikra za kimkakati zinahitaji uwezo wa kubadilika kulingana na mazingira, kusikiliza mitazamo tofauti na kuhoji mazoea au imani ambazo watu wengi huzichukulia kama ukweli wa kawaida.

Katika biashara, viongozi wasiofikiri kimkakati mara nyingi hushughulikia "moto wa kila siku" bila kujiandaa kwa mabadiliko ya soko, teknolojia au tabia za wateja.

Kwa mtu binafsi pia, maisha yasiyo na fikra za kimkakati yanaweza kujaa maamuzi ya haraka yasiyo na dira ya muda mrefu.

## Mwelekeo wa kimkakati (Strategic direction)

Baada ya kuwa na fikra pana, hatua inayofuata ni kujua nini hasa ni muhimu.

Changamoto kubwa ya dunia ya sasa si ukosefu wa fursa pekee, bali wingi wa kelele, taarifa na mambo ya kufanya. Ndiyo maana watu na taasisi nyingi hujikuta zikiwa na shughuli nyingi lakini maendeleo kidogo.

Mwelekeo wa kimkakati unahusu kuchagua mambo muhimu zaidi na kuacha mengine.

Hii inahitaji kufanya maamuzi magumu na wakati mwingine kukubali kuwa huwezi kufanya kila kitu kwa wakati mmoja. Wataalamu wa biashara husema kuwa mkakati mzuri si tu kujua nini cha kufanya, bali pia kujua nini usifanye.

Katika timu au taasisi, mwelekeo wa pamoja huwasaidia watu kufanya kazi kwa lengo moja badala ya kila mtu kwenda kivyake.

## Mipango ya kimkakati (Strategic planning)

Ndoto au maono pekee havitoshi bila mpango wa utekelezaji.

Mipango ya kimkakati inahusu kuvunja malengo makubwa katika hatua ndogo zinazoeleweka. Hapa ndipo watu huamua kazi itafanyikaje, ni nani atafanya nini na ni mfumo gani utatumika. Wataalamu wanaeleza kuwa taasisi nyingi hushindwa si kwa sababu ya kukosa maono, bali kwa sababu ya kukosa mifumo mizuri ya kazi.

Mipango mizuri huweka sheria za kazi, ratiba, vipaumbele na njia za kupima maendeleo. Pia huwasaidia watu kupunguza mkanganyiko na matumizi mabaya ya muda na rasilimali.

Kwa mtu binafsi, mipango ya kimkakati inaweza kujumuisha kuweka ratiba za fedha, masomo, biashara au maendeleo binafsi badala ya kuishi kwa maamuzi ya kubahatisha kila siku.

## Utekelezaji wa kimkakati (Strategic execution)

Msingi wa mwisho na muhimu zaidi ni utekelezaji. Watu wengi wana mawazo mazuri na mipango mizuri, lakini wachache wana nidhamu ya kutekeleza kwa mwendelezo. Wataalamu wanasema mafanikio makubwa mara nyingi hutokana si na motisha ya muda mfupi, bali tabia zinazojirudia kila siku.

Utekelezaji wa kimkakati unahusisha mawasiliano ya wazi, kujenga utaratibu wa kazi unaoeleweka na kuimarisha viwango vinavyotarajiwa.

Katika taasisi, viongozi wanapaswa kuwa mfano wa tabia wanazotaka kuona kwa wengine. Katika maisha binafsi pia, mafanikio hujengwa zaidi na tabia za kila siku kuliko malengo yanayoandikwa mwanzoni mwa mwaka halafu kusahaulika.

Mwisho wa siku, mkakati si karatasi ya mipango wala maneno ya motivasheni pekee. Ni uwezo wa kufikiri kwa upana, kuchagua muhimu, kupanga kwa umakini na kutekeleza kwa nidhamu kila siku.

Afya
Pure Drinking water

"Afya"is natural source of sweet drinking water from underground stream which is blended with essential minerals to support and aid perfect metabolism.

WATERCOM LIMITED
P.o. Box 20409, Plot N.4005, Kisarawe11 area Temeke, Dar es Salaam, Tanzania. www.watercomtz.com, Email:info@watercomtz.com



Na Junaynat Ally Dama
0789 201 383

# Wauguzi: Moyo wa kibinadamu unaoubeba mfumo wa afya



Mashujaa wengi hawavai makoti ya kifalme. Huvaa sare za uuguzi, viatu vya kazi na tabasamu lililofichwa nyuma ya uchovu wa zamu ndefu hospitalini.

Kila mwaka dunia huadhimisha Wiki ya Wauguzi kuanzia Mei 6 hadi 12, lakini nyuma ya pongezi hizo kuna ukweli mmoja mkubwa ambao mara nyingi hausikiki: bila wauguzi, mfumo wa afya unaweza kusimama.

Wauguzi ndio wanaokaa karibu zaidi na wagonjwa kuliko kada nyingine yoyote ya afya, wakiitikia dharura na mara nyingi ndio wa mwisho kumuona mgonjwa kabla ya zamu kuisha.

Daktari anaweza kufanya uchunguzi, kusoma vipimo na kuandika dawa, lakini ni muuguzi anayebaki pembeni ya kitanda kwa saa nyingi akihakikisha mgonjwa anakula, anapata dawa kwa wakati na hali yake haibadiliki ghafla. Katika hospitali nyingi, ndugu hawaruhusiwi kulala wodini na wagonjwa. Nafasi hiyo hubebwa na wauguzi.

## Uuguzi hauishii kwenye sindano au dawa.

Wauguzi huwafariji wagonjwa kabla ya upasuaji, hukaa na familia wakati wa taarifa mbaya na huwapa matumaini watu wanaoogopa kufa. Mara nyingi hubeba huzuni za wagonjwa na familia zao huku wakijitahidi kubaki watulivu.

Huduma ya uuguzi imejengwa kwenye huruma, ubinadamu na uwepo wa karibu kwa mgonjwa. Katika moja ya simulizi zilizochapishwa na HCA Healthcare, muuguzi mmoja nchini Marekani aliokoa maisha ya jirani yake baada ya moyo wake kusimama usiku wa manane. Aliendelea kufanya huduma ya uokoaji wa moyo (CPR) kwa dakika karibu nane hadi wahudumu wa dharura walipofika.

Hata hivyo, uuguzi ni kada inayojipambanua kwa changamoto zake nyingi, hasa Afrika.

Kwa mujibu wa Médecins Sans Frontières wakinukuliwa AllAfrica, nchi maskini zina wastani wa wauguzi chini ya 10 kwa kila watu 10,000, wakati nchi tajiri zina zaidi ya wauguzi 100 kwa idadi hiyo hiyo. Hii ina maana kuwa wauguzi wengi Afrika wanahudumia wagonjwa wengi kupita uwezo wao.

Baadhi hufanya kazi katika mazingira yenye vita, njaa, uhaba wa dawa na vifaa tiba huku wao wenyewe wakiwa sehemu ya jamii zinazoteseka. Jean Stowell wa MSF anasema jambo linalowatofautisha wauguzi ni uwezo wao wa kuendelea kuwa na ubinadamu licha ya trauma wanazoziona kila siku.

"Ni wauguzi wanaowafuata wagonjwa hawa kila siku. Wanaona mateso mengi, lakini bado wanaendelea kuwa na huruma," alisema.

## Wito wa maisha

Uuguzi si kazi ya mshahara pekee, bali wito wa maisha. Muuguzi mmoja, akinukuliwa katika makala katika tovuti ya Chuo Kikuu cha Victoria anayehudumia wagonjwa wanaokaribia kufariki alisema kazi yake ni kuwa karibu na watu katika nyakati zao dhaifu zaidi.

Katika huduma za mwisho wa maisha (palliative care), wauguzi hawahangaikii tu kuongeza siku za kuishi, bali kuhakikisha mgonjwa anabaki na heshima, utulivu na faraja mpaka mwisho wa maisha yake.

Lakini licha ya umuhimu huo, mfumo wa afya duniani unaendelea kupoteza wauguzi.

Takwimu zilizochapishwa kwenye tovuti ya Detroit News, karibu muuguzi mmoja kati ya wanne huacha kazi yake ya kwanza ndani ya mwaka mmoja. Sababu kubwa ni uchovu wa kazi (burnout), mzigo mkubwa wa wagonjwa, uhaba wa watumishi na msongo wa mawazo.

Makala hiyo inaeleza kuwa wauguzi wengi wapya huingia hospitalini wakiwa na elimu, nguvu na ndoto za kusaidia wagonjwa, lakini ndani ya muda mfupi hukutana na mazingira magumu kuliko walivyotarajia.

"Uvumilivu pekee hauwezi kuwa suluhisho la kuwabakiza wauguzi kazini," linaeleza andiko hilo.

## Wauguzi hawapati usaidizi wa AI

Katika dunia inayozidi kutegemea teknolojia na akili mnemba (Artificial Intelligence – AI), baadhi ya kazi za kitabibu zinaweza kusaidiwa na mashine. AI inaweza kusaidia kusoma vipimo na kufanya uchambuzi wa taarifa za afya. Lakini ni vigumu AI kuchukua nafasi ya muuguzi.

Mashine haiwezi kushika mkono wa mgonjwa mwenye hofu, kumbembeleza mtoto anayelia wodini au kugundua kupitia uso wa mgonjwa kuwa hali yake inaanza kubadilika kabla hata vipimo havijaonyesha tatizo.

Wataalamu wa afya wanasema kazi kubwa ya muuguzi mara nyingi haionekani kwa sababu sehemu kubwa ya kazi yao ni kuzuia hali isiharibike. Wagonjwa wengi hupona bila kujua ni mara ngapi muuguzi aliokoa maisha yao kimya kimya.

Ndiyo maana wataalamu wanaamini kuwa kuwasifia wauguzi kwa siku moja haitoshi kama mazingira yao ya kazi bado ni magumu. Wanahitaji si tu pongezi, bali pia mazingira bora ya kazi, msaada wa afya ya akili, mishahara inayostahili na idadi ya kutosha ya watumishi.

Hospitali zinaweza kuwa na vifaa vya kisasa na madaktari bingwa, lakini wauguzi ndio wanaofanya huduma za afya zibaki na moyo wa kibinadamu.

Mikono yao hutibu, lakini mioyo yao huifariji dunia.

ذو الحجة

**MAKALA MAALUM**

**SEHEMU YA 1**

Na Said Rajab
0783 650 803



# Waislamu walivyopoteza dira yao!

**Historia haifunguki kwa ghafla, wala madola hayaanguki kwa pigo moja. Badala yake, anguko huanza pale dira ya kisiasa inapokengeuka kutoka katika msingi wake wa kiitikadi, bila kujali majina na kauli mbiu zinazobaki. Katika Uislamu, dola si utawala wa dhahania (abstract), wala mamlaka inayotafuta kuendeleza uhai wake yenyewe, bali ni mamlaka yenye jukumu la kutekeleza Uislamu ndani ya nchi na kueneza ujumbe huo katika medani ya kimataifa.**

Katika zama za Makhalifa waongofu, utawala ulikuwa mfano halisi wa maana ya bay'a (kiapo cha utii kwa utawala). Katika zama hizo, mamlaka haikuwa mali ya watu binafsi, bali ilikuwa ya umma mzima.

Mtawala hakuwa juu ya sharia; alitumika kama chombo cha kusimamisha Dini ya Mwenyezi Mungu na kusimamia mambo ya umma kwa mujibu wa hukumu za sharia. Hivyo, uimara wa dola ulitokana na uwazi wa itikadi yake, na si nguvu ya silaha zake.

Mabadiliko yaliyotokea katika baadhi ya vipindi vya kihistoria hayakuwa tu ya kubadilika kwa watawala, bali yaliathiri mfumo mzima wa uhamishaji wa mamlaka na uhusiano kati ya umma na mtawala.

Utawala ulipogeuzwa kuwa wa kinasaba na wa kung'ang'ania madaraka, mifumo ya uwajibikaji wa kisiasa ilianza kudhoofika. Ukabila ukaibuka na dosari za kimuundo zikaanza kujitokeza.

Ingawa sharia ya Kiislamu haikutoweka katika jamii, na ufunguzi wa ardhi mpya kwa ajili ya Uislamu haukusimama, roho ya mfumo wa kisiasa ilianza kupoteza usafi wake wa awali. Tatizo kubwa lilikuwa katika muundo wa mfumo wenyewe.

Utawala unapoacha kutegemea bay'a na badala yake kujengwa juu ya unyakuzi au urithi wa madaraka, dhana ya mamlaka ya mtawala juu ya umma hupungua, hata kama istilahi zinazotumika ni zilezile.

Kadri muda unavyopita, pengo kati ya mtawala na umma huongezeka. Utawala hubadilika kutoka kuwa mfumo wa kusimamia mambo ya umma na kuwa utawala wa urasimu, na mwishowe hutoka katika kubeba ujumbe wa Uislamu (Risalah) na kugeuka kuwa chombo cha kugombania madaraka.

Mmomonyoko huu wa ndani uliifanya dola ya Kiislamu kuwa katika hatari kubwa zaidi mbele ya mashambulizi ya kigeni. Vita vya Msalaba na uvamizi wa Wamongolia havikuwa chanzo kikuu cha udhaifu huo, bali vilikuwa matokeo ya udhaifu wa ndani wa dola ya Kiislamu.

Umma wenye maono ya wazi na uongozi wenye mshikamano ni vigumu kuupenya. Lakini watu wanapojishughulisha na kugombania madaraka, huku umuhimu wa kueneza ujumbe wa Uislamu ukipungua na kuacha kuwa lengo kuu, asili ya dola hubadilika kutoka kuwa chombo cha kuuongoza umma na kuwa taasisi inayopigania uhai wake yenyewe.

Hata hivyo, kulijitokeza juhudi za kurekebisha hali hiyo kwa lengo la kurejesha dhana ya dola kama chombo cha msingi cha kubeba ujumbe wa Kiislamu duniani.

Khalifa Nur ad–Din Mahmud pamoja na kamanda wake wa kijeshi, Salahuddin Al–Ayubi walionesha njia ambayo mradi wao haukuwa tu wa ukombozi wa ardhi, bali pia wa kurejesha umoja wa umma na maono yake.

*Itaendelea wiki ijayo, Insha Allah.*

ذو الحجة

**TUJIFUNZE**

**AI (ARTIFICIAL INTELLIGENCE)**

Na Junaynat Ally Dama

SEHEMU YA 2

# Jinsi akili bandia (AI) inavyo badilisha dunia



Mabadiliko yanayoletwa na akili bandia hayaishii katika nadharia au matarajio ya baadaye; tayari yanaonekana katika soko la ajira. Tofauti na mapinduzi ya awali ya kiteknolojia, safari hii kasi ni kubwa na athari zake zinafika moja kwa moja katika kazi nyingi za kila siku. Swali la msingi sasa si kama ajira zitabadilika, bali ni kwa kiwango gani, na ni nani atakayebaki salama.

Tafiti kadhaa zinaonyesha ukubwa wa mabadiliko haya. Ripoti ya benki ya uwekezaji ya Goldman Sachs inakadiria kuwa AI inaweza kuchukua nafasi ya ajira zinazolingana na wafanyakazi milioni 300 duniani. Hii haimaanishi watu wote hao watapoteza kazi mara moja, bali inaashiria kiwango cha kazi kinachoweza kufanywa na mashine badala ya binadamu. Kwa mtazamo huo, karibu theluthi mbili ya kazi katika baadhi ya maeneo zinaweza kuathiriwa kwa namna fulani na otomatiki.

Kinachovutia zaidi ni aina ya kazi zinazoguswa. Tofauti na ilivyokuwa zamani ambapo kazi za mikono ndizo zilikuwa hatarini, sasa hata kazi za kitaaluma zenye mishahara ya kati na ya juu zinaanza kuguswa.

Utafiti uliofanywa na watafiti kutoka Chuo Kikuu cha Pennsylvania na OpenAI unaonyesha kuwa wafanyakazi wa ofisini—hasa wale wanaofanya kazi za uchambuzi wa maandishi, taarifa na data—wako katika hatari kubwa ya kuathiriwa na AI.

Kazi nyingi zilizo katika hatari zina sifa moja kuu: zinajirudia na zinafuata kanuni maalum. Huduma kwa wateja ni mfano wa wazi. Kwa miaka mingi, kampuni zimekuwa zikitegemea wafanyakazi kujibu maswali ya wateja. Lakini leo, mifumo ya AI inaweza kujibu maswali hayo kwa haraka zaidi, bila makosa mengi, na kwa gharama ndogo.

Hali ni hiyo hiyo kwa wahudumu wa mapokezi, ambapo roboti na mifumo ya sauti imeanza kuchukua nafasi ya binadamu katika kupokea wageni na kupokea simu.

Katika sekta ya uhasibu, programu zinazotumia AI zina uwezo wa kukusanya, kuchambua na kuhifadhi taarifa za kifedha kwa usahihi mkubwa. Kazi ambazo hapo awali zilihitaji saa nyingi za binadamu sasa zinaweza kufanyika ndani ya sekunde chache. Vivyo hivyo, katika mauzo na masoko, majukwaa ya mitandao ya kijamii yamebadilisha kabisa mfumo wa matangazo. Badala ya wauzaji wa ana kwa ana, sasa kampuni zinatumia algorithimu kufikia wateja kulingana na tabia zao mtandaoni.

Sekta ya utafiti na uchambuzi wa data pia inaathirika. Kompyuta za kisasa zina uwezo wa kuchambua mamilioni ya rekodi kwa muda mfupi, kugundua mifumo (patterns) ambayo binadamu angehitaji muda mrefu kuitambua. Hii inaibua swali la msingi: je, nafasi ya mchambuzi wa data itabaki kuwa ile ile katika miaka ijayo?

Katika maghala na usafirishaji, otomatiki inaendelea kubadilisha jinsi kazi zinavyofanyika. Mifumo ya kompyuta inaweza kufuatilia bidhaa, kupanga mizigo, na hata kuongoza roboti kufanya kazi za kupakia na kupakua. Hata katika sekta ya bima, tathmini za hatari zinazotegemea data sasa zinaweza kufanywa na AI kwa ufanisi zaidi kuliko binadamu.

Hata hivyo, picha hii si ya upande mmoja. Ingawa kazi nyingi ziko hatarini, pia kuna dalili kwamba AI itachochea ukuaji wa ajira mpya. McKinsey inakadiria kuwa hadi asilimia 14 ya wafanyakazi duniani wanaweza kulazimika kubadilisha taaluma zao ifikapo mwaka 2030. Hii inaonyesha kuwa changamoto kubwa si kupotea kwa ajira pekee, bali ni mabadiliko ya aina ya ajira.

Kwa maneno mengine, tatizo si kwamba kazi zitapotea, bali kwamba mahitaji ya ujuzi yatabadilika kwa kasi ambayo si kila mtu yuko tayari kuendana nayo. Hapa ndipo pengo la ujuzi (skills gap) linapojitokeza—tofauti kati ya ujuzi uliopo na ujuzi unaohitajika katika soko jipya la ajira.

Kwa mtazamo mpana wa uchumi, AI inaonekana kuongeza uzalishaji na ufanisi. Lakini ongezeko hilo linaweza kuja na changamoto za kijamii, hasa kama watu wengi watabaki bila ujuzi unaohitajika katika soko jipya. Hivyo, swali la ajira halipaswi kuangaliwa pekee yake; linahusiana moja kwa moja na elimu, mafunzo, na sera za kijamii.


Kwa kifupi, dunia inaingia katika kipindi ambacho kazi nyingi zitafanywa kwa njia tofauti kabisa na tulivyozoea. Baadhi ya kazi zitapungua au kutoweka, nyingine zitabadilika, na mpya zitaibuka. Changamoto kwa mtu mmoja mmoja si tu kutafuta ajira, bali kuhakikisha ana ujuzi unaolingana na mahitaji ya wakati.

MUSSA IMANI SHEHA ZANZIBAR
0773 181 494

SEHEMU YA 8




# SIMULIZI YA MTUME MUSA (AMANI YA ALLAH IMSHUKIE)



## VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

**Katika toleo la wiki iliyopita tuliona Allah alimtuma Musa kwa Fir-aun na watu wake huku akimtaka nabii wake huyu asiwe na hofu yoyote ya kudhuriwa na maadui wake.**
**Aidha, Musa alikumbushwa neema na hifadhi ya Mwenyezi Mungu juu yake tokea alipokuwa mtoto mchanga na kuhakikishiwa kwamba, ataendelea kuwa katika uangalizi wa Muumba wake na hivyo hakutakuwa na ovu lolote litakalomfika katika majukumu yake ya kuifikisha risala (ujumbe) kwa watu.**

### Nabii Musa na Harun mbele ya Fir-aun na wakuu wenzake

Mtume Musa na ndugu yake Harun (Amani iwe juu yao) waliagizwa na Mola wao waseme na Fir-aun kwa maneno laini huenda atawaelewa na kuonyeka. Walipofika wakamwambia: "..sisi ni wajumbe wa mola wako, basi waachie wana wa Israil watoke pamoja nasi na usiwaadhibu, hakika tumekuletea ishara zitokazo kwa mola wako, na Amani itakuwa juu ya watakaofuata uongofu. Sisi tumeletewa wah-I (tumefunuliwa) yakwamba, adhabu itawasibu (itawapata) watakaopinga na kuyapa mgongo (maonyo)." [Qur'an, 20:27-28].

### Majibu ya Fir-aun kwa Mitume wa Allah

Ujasiri wa Musa na kujiamini kwake wakati wa kuuwasilisha ujumbe huu kwa mara ya kwanza, kulimkasirisha sana Fir-aun na kumpandisha kiburi.

Fir-aun akasema: "Je hatukukulea kwetu (ulipokuwa) mtoto na ukakaa kwetu miaka mingi ya umri wako? Na ukafanya kitendo (cha kumua mtu) na ukawa miongoni mwa waliokosa shukurani? [Qur'an, 26:18-19].

Mtume Musa wala hakukasirika na majibu ya ukali ya Fir-aun, bali –kwa utulivu- alisema: "Niliyafanya hayo nilipokuwa miongoni mwa wasiojua. Basi nikakukimbieni (nikakutorokeni) nilipokuogopeni (msije kuniua). Mola wangu amenipa sasa hukumu na amenijaalia kuwa mtume. Na hiyo ndiyo neema uliyonipatia ya kunisumbulia iwe ndio sababu ya kuwatia utumwani Wana wa Israil?" [Qur'an, 26:20-22].

### Maelezo

Hapa Mtume Musa (amani ya Allah imshukie) anamwambia adui yake (Fir-aun) kwamba hayo mema anayojigambia ya kumfanyia hayalingani hata kidogo na uovu aliowafanyia ndugu zake (Wana wa Israil) wa kuwafanya watumwa, kuwatesa na kuwaulia vijana wao.

Musa alijenga hoja kuwa lau si amri yake ya kuwaua watoto wa kiume, kamwe mama yake asingelimtosa kwenye mto, na kamwe asingelifika kuokotwa na kulelewa katika jumba lake.

Kuanzia hapa ulianza kuonekana udhaifu wa mtawala huyo katika kujenga hoja kwani alitoka kwenye hoja hiyo haraka na kuhamia kwenye hoja nyengine. Na hapa mjadala mkali ukaanza. Twende katika Surat Shuraa (28) tukaone mapambano hayo ya hoja.

"(Fir-an) akasema, 'Na nani huyo Mola wa walimwengu?' (Musa) akasema, 'Muumba wa mbingu na ardhi na vilivyo ndani yake ikiwa nyinyi ni wenye yakini (ya jambo, basi yakinisheni hili).' Fir-aun akawaambia waliomzunguka, 'Je mnasikia (maneno ya mpuuzi huyu?' (Musa) akasema, '(Mungu huyo) ndiye Mola wenu na Mola wa baba zenu waliotangulia.' (Fir-aun) akasema, 'Bila shaka mtume wenu aliyetumwa kwenu ni mwendawazimu.' (Musa akaangusha hoja nyengine) akasema, '(Huyo ndiye) Mola wa mashariki na magharibi na vilivyo baina yake ikiwa mnafahamu (jambo mtafahamu hili).'" [Qur'an, 26:23-28].

Katika sura nyengine, [Qur'an, 20:49-55], mapambano haya yanaelezwa kama ifuatavyo:

"(Fir-aun) akasema, 'Na ni nani huyo Mola wenu ewe Musa?' Akasema, 'Mola wetu ni ambaye amekipa kila kitu umbo lake kisha akakiongoza.' (Fir-aun) akasema, 'Nini hali za karne za kwanza?'

(Musa) akasema, 'Ilimu yake iko kwa Mola wangu katika kitabu chake, Mola wangu hapotei wala hasahau. Ambaye amekufanyieni ardhi kuwa tandiko na akakuwekeeni humo njia na akayateremsha maji kutoka mawinguni, na kwa hayo akaotesha aina mbali mbali za mimea, kuleni na walisheni wanyama wenu, bila shaka katika hayo zimo ishara kwa wenye akili za kuzingatia. Katika hii ardhi tumekuumbeni, na humo tutakurudisheni, na kutoka humo tutakutoweni mara nyingine (muwe hai tena)." [Qur'an, 20:49-55].

### Mazingatio:

Aya zote tulizozirejea zinatuonesha mtanange (mashindano) ya mwanzo pale Musa alipokutana na Fir-aun tangu kupokea utume kutoka kwa Mola wake.

Tumeona Mtume Musa na ndugu yake (Haruna, Amani ya Allah ziwe juu yao) namna walivyomshushia Fir-aun na mawaziri wake hoja na nukuu nzito, zilizomshinda kuzipangua, akaonekana kubabaika, huku akitaka kuwaaminisha waliomzunguka eti maneno ya Musa ni ya kipuuzi na ya kiwendawazimu.

Hoja za Mitume hao watukufu zililenga kuvunja madai ya uungu wa Fir-aun, kumtambulisha Allah mbele yake na Upweke wake katika uumbaji na uendeshaji viumbe.

*Itaendelea inshaAllah*

ذو الحجة

**MAKALA YA AFYA**

Na Junaynat Ally Dama

# Bangi yahusishwa na hatari ya mimba kutoka

Matumizi ya bangi yanaweza kuathiri afya ya uzazi kwa kiwango kikubwa kuliko watu wengi wanavyodhani. Wataalamu wa afya sasa wanaonya kuwa bangi inaweza kuharibu ubora wa mbegu za kiume, kuongeza uwezekano wa mimba kutoka na kuchangia ugumu wa kupata watoto.

Tahadhari hiyo ilitolewa katika mahojiano kati ya Dkt. Andrew Huberman na Dkt. Natalie Crawford kwenye kipindi cha Huberman Lab Podcast.

Dkt. Huberman ni mwanasayansi wa neva (neuroscientist) na profesa katika Idara ya Neurobiology ya Chuo Kikuu cha Stanford nchini Marekani. Dkt. Crawford ni daktari bingwa wa afya ya uzazi wa wanawake (OB-GYN) pamoja na mtaalamu wa homoni na matatizo ya uzazi (reproductive endocrinologist).

Kwa mujibu wa Dkt. Crawford, matumizi ya bangi yana madhara makubwa kwa afya ya uzazi wa mwanaume, kuanzia uzalishaji wa mbegu za kiume hadi ubora wa DNA ndani ya mbegu hizo.

"Matumizi yote ya bangi yana madhara makubwa kwa afya ya uzazi. Huathiri uzalishaji wa mbegu za kiume, idadi yake, homoni ya testosterone pamoja na ubora wa mbegu hizo, hasa uharibifu wa DNA," alisema.

Alieleza kuwa hata mwanaume akiwa bado ana uwezo wa kumpa mwanamke ujauzito, bangi inaweza kuwa tayari imeharibu ubora wa mbegu zake bila dalili kuonekana mapema.

Kwa mujibu wa Dkt. Crawford, wanawake wanaopata ujauzito kutoka kwa wanaume wanaotumia bangi huwa katika hatari kubwa zaidi ya mimba kutoka.

"Wanawake wanaopata ujauzito kutoka kwa wanaume wanaotumia bangi wana viwango vya juu zaidi vya mimba kutoka kuliko wale ambao wenza wao hawatumii bangi," alisema.

Katika maabara za upandikizaji wa mimba (IVF), wataalamu wamekuwa wakiona viinitete vikishindwa kuendelea kukua siku ya tatu baada ya urutubishaji. Kwa mujibu wa Dkt. Crawford, hali hiyo mara nyingi huhusishwa na matumizi ya bangi kwa mwanaume.

"Tunapofuatilia kwa undani, mara nyingi tunagundua mwanaume alikuwa anatumia bangi, hata kama hapo awali alikuwa amekataa," alisema.

Mbali na ushuhuda huo wa kitabibu, tafiti mbalimbali zimeonyesha uhusiano kati ya bangi na matatizo ya uzazi. Utafiti mmoja wa mwaka 2015 uliohusisha wanaume 1,215 nchini Denmark ulibaini kuwa waliokuwa wakitumia bangi zaidi ya mara moja kwa wiki walikuwa na asilimia 28 ya upungufu wa msongamano wa mbegu za kiume na asilimia 29 ya upungufu wa jumla ya mbegu hizo.

Tafiti nyingine zimeonyesha kuwa kemikali ya THC iliyopo kwenye bangi inaweza kuharibu DNA ya mbegu za kiume. Watafiti wanaamini hali hiyo inaweza kuathiri ukuaji wa kijusi na kuongeza hatari ya ujauzito kuharibika.


Wataalamu pia wanaonya kuwa bangi za sasa zina kiwango kikubwa zaidi cha THC kuliko ilivyokuwa miaka ya nyuma, jambo linaloongeza wasiwasi kuhusu madhara yake kwa afya ya uzazi.

Hata hivyo, kuna habari inayotoa matumaini. Wataalamu wanaeleza kuwa madhara mengi ya bangi kwenye mbegu za kiume yanaweza kupungua baada ya mtu kuacha matumizi yake.

Kwa mujibu wa tafiti, uzalishaji wa mbegu za kiume huchukua siku 70 hadi 90. Hivyo, mwanaume anayeacha bangi anaweza kuanza kuona maboresho ya ubora wa mbegu zake baada ya takribani miezi mitatu.

Utafiti mmoja wa mwaka 2021 pia ulibaini kuwa baadhi ya mabadiliko kwenye DNA ya mbegu za kiume yaliyosababishwa na bangi yalipungua baada ya kipindi hicho cha kuacha matumizi.

Madaktari wanashauri wanaume wanaotarajia kupata watoto kuacha bangi angalau miezi mitatu kabla ya kuanza kutafuta ujauzito. Pia wanasisitiza umuhimu wa lishe bora, usingizi wa kutosha, mazoezi na kuepuka sigara pamoja na pombe kupita kiasi.



MATUKIO YENYE MAZINGATIO

NA ZAHARANI BARAKA

ذُو الحِجَّة

**Kutoka kwa Abu Huraira (Allah amridhie) amesimulia kuwa, siku moja mjumbe wa Allah (rehema na amani zimshukie) aliwahutubia akasema: "Enyi watu! Hijja imefaradhishwa kwenu, basi hijini." Mtu mmoja akauliza: "Je, (tuhiji) kila mwaka ewe mjumbe wa Allah?"**

**Mtume (rehema na amani zimshukie) akanyamaza hadi mtu yule aliporudia swali hilo mara tatu, kisha akasema: "Kama ningesema 'Ndiyo', mngelazimika (mngefaradhishwa kuhiji kila mwaka) na msingeweza."**

**Mtume akaendelea kusema: "Niacheni katika yale niliyokuachieni, kwani waliokuwa kabla yenu waliangamia kwa sababu ya kuuliza maswali mengi na kupingana na Mitume wao. Nikikuamrisheni jambo lifanyeni kadri mnavyoweza, na nikikukatazeni jambo jiepusheni nalo."**

***[Bukhari]***

# Nafasi ya Hijja katika kuimarisha umoja na maadili

## fundisho ya tukio

Hijja ni ibada inayoonesha ukamilifu wa imani na kujisalimisha kwa Allah. Pia ni ibada inayowapa waumini fursa ya kujitakasa na madhambi. Mtume amesema: "Atakayehiji na akawa hakusema wala kufanya mambo maovu au maasi, atarejea kama siku aliyozaliwa na mama yake (yaani bila ya dhambi yoyote)." [Bukhari na Muslim].

Utakaso huu humpa Muislamu mwanzo mpya usio na mzigo wa madhambi, jambo linaloathiri vyema maisha yake ya kiroho, kimwili na kiakili.

## Fursa ya kutubia

Ibada ya Hijja humpa Muislamu nafasi ya kujitathmini, kutubia madhambi na kufikiria upya ahadi yake ya utiifu kwa Allah, jambo linaloongeza imani na usafi wa kiroho.

Katika mazingira ya Hijja yaliyojaa unyenyekevu na utulivu wa ibada, nyoyo hupokea nuru ya uongofu huku nafsi zikisafishwa kutokana na uchafu wa dunia.

Umuhimu wa Hijja katika Uislamu huonekana wazi kupitia mamilioni ya Waislamu wanaokusanyika sehemu moja bila kujali tofauti za rangi, lugha, makabila au mataifa, huku wakiunganishwa na vazi moja, ibada moja na lengo moja la kumkaribia Allah.

Katika mandhari hiyo tukufu, ukubwa wa Uislamu na umoja wa Umma hujitokeza wazi katika nyanja za kiroho, kijamii, kimaadili na hata kiuchumi.

## Somo la umoja, uvumilivu na usawa

Hijja ni kielelezo cha umoja na usawa wa Waislamu, kwani huwakutanisha waumini kutoka pembe zote za dunia bila kujali rangi, lugha au mataifa wanayotoka. Katika ibada hii, mahujaji wote huvaa vazi moja la Ihram na kutekeleza ibada zinazofanana katika mazingira yanayodhihirisha usawa wa kweli mbele ya Allah Mtukufu.

Aidha, Hijja huwafundisha Waislamu subira, nidhamu, unyenyekevu na kuidhibiti nafsi dhidi ya mambo yaliyokatazwa. Pia huwakumbusha umuhimu wa kujiepusha na matamanio, kuvumilia changamoto na kujikurubisha kwa Allah.

## Safari ya kukumbuka historia

Hijja, pia ni ibada inayohuisha kumbukumbu za Nabii Ibrahim na mwanawe Ismail (amani iwashukie) kupitia matendo ya kusai, kutufu na kurusha vijiwe.

Huu ni ukumbusho kwa Waislamu kuhusu historia ya Mitume na kujitolea kwao katika kueneza dini na kuifanyia kazi. Vilevile ni mwaliko wa kujifunza kujitoa kwa ajili ya Allah na kujisalimisha kwake.

## Kutukuza alama za Allah

Kutekeleza ibada ya Hijja ni miongoni mwa alama kubwa za kumtukuza Allah 'Azza Wajallah'. Allah anasema: "Na anayezitukuza alama za Mwenyezi Mungu, basi hilo ni katika uchamungu wa nyoyo." [Qur'an, 22:32].

Kupitia Hijja, Muislamu huonesha utiifu wake kamili kwa Allah na kuheshimu alama na ishara zake.

## Umoja na udugu wa Kiislamu

Ibada ya Hijja ni fursa muhimu ya kuimarisha umoja wa Kiislamu, kutambuana, kubadilishana uzoefu pamoja na tamaduni mbalimbali, hivyo kujenga uhusiano mwema wa kidini na kijamii hata baada ya Hijja kumalizika. Vilevile, Hijja huimarisha mshikamano wa kindugu kupitia matendo ya kusaidiana, ikiwamo kuchinja wanyama wa hadyi siku ya Idi na kuwasaidia wahitaji.

Hijja, pia huchangia mabadiliko ya tabia kwa mahujaji wengi ambapo hushikamana zaidi na maadili ya Kiislamu pindi wanaporejea kwenye miji yao. Jamii huwatazama kwa jicho tofauti baada ya kutekeleza ibada hiyo, jambo linalosaidia kueneza tabia njema katika familia na jamii kwa ujumla.

JUNAYNAT ALLY DAMA

ذو الحجة

# Watoto wana lugha tofauti za kupendwa – je, unaielewa ya mtoto wako?



Wazazi wengi huwapenda watoto wao kwa dhati, lakini si watoto wote wanaelewa upendo kwa njia moja. Mtoto mmoja anaweza kujisikia kupendwa kupitia maneno mazuri, mwingine kupitia muda wa kuwa pamoja, na mwingine kupitia kukumbatiwa.

Ndiyo maana wakati mwingine mzazi anaweza kujitahidi sana kwa ajili ya mtoto wake, lakini mtoto bado akahisi kama hapendwi vya kutosha. Kwa mujibu wa mwanasaikolojia na mshauri wa familia Gary Chapman, watoto wana "lugha tano za upendo" (five love languages) — yaani njia kuu wanazotumia kuelewa kuwa wanapendwa.

Wataalamu wa saikolojia ya watoto wanasema hitaji la kupendwa ni moja ya mahitaji muhimu zaidi kwa mtoto. Mtoto anayehisi kupendwa na kuthaminiwa huwa na nafasi kubwa ya kukua akiwa na utulivu wa kihisia, kujiamini na uwezo mzuri wa kujenga mahusiano baadaye maishani.

## Maneno ya kuthamini (Words of affirmation)

Kwa baadhi ya watoto, maneno yana nguvu kubwa sana. Kauli kama "Ninajivunia wewe," "Umejitahidi sana," au "Una akili na ubunifu" huwajenga ndani kwa ndani.

Kwa mujibu wa maelezo ya Gary Chapman, watoto wenye lugha hii ya upendo huhitaji kusikia maneno ya kutia moyo na kuthaminiwa mara kwa mara.

Wataalamu wanaeleza kuwa watoto hawa huumia sana wanapokosolewa kupita kiasi au wanapoishi kwenye mazingira yenye maneno makali. Kwao, maneno yanaweza kujenga au kubomoa moyo.

Mzazi anaweza kuonyesha upendo kwa kuandika ujumbe mdogo kwenye daftari la mtoto, kumpongeza mbele ya wengine au kumwambia kila siku kuwa anampenda.

## Kuguswa na kukumbatiwa (Physical touch)

Watoto wengine huhisi upendo kupitia mguso wa karibu — kukumbatiwa, kubebwa, kushikwa mkono au hata kupigwa "high five."

Wataalamu wa malezi wanasema watoto wanaopata mguso wa upendo mara nyingi hujenga hisia kubwa ya usalama wa kihisia.

Kwa mtoto mwenye lugha hii ya upendo, mzazi anayekaa karibu naye, anayempigapiga mgongoni kwa upole au anayemkumbatia kabla ya kulala huwa anatuma ujumbe mkubwa kuliko maneno mengi.

Gary Chapman anaeleza kuwa hata watoto wanapokuwa wakubwa au kuingia balehe, bado wanahitaji mguso wa upendo unaofaa.

## Muda wa pamoja (Quality time)

Kwa baadhi ya watoto, upendo ni muda.

Mtoto anaweza asiwe na shida ya zawadi wala maneno mengi, lakini akajisikia kupendwa sana mzazi anapokaa naye bila simu, televisheni au usumbufu mwingine.

Kwa mujibu wa wataalamu, muda wa pamoja si lazima uwe safari kubwa au matumizi makubwa ya fedha. Wakati mwingine ni mazungumzo ya dakika chache kabla ya kulala, kutembea pamoja au kucheza mchezo mmoja mezani.

Watoto wengi hulalamika kuwa wazazi wao wako karibu kimwili lakini mbali kihisia kutokana na simu, kazi au shughuli nyingi.

Kwa mtoto mwenye lugha hii ya upendo, umakini wa mzazi ni zawadi kubwa kuliko vitu vya gharama.

## Zawadi (Gifts)

Watoto wengine huhisi kupendwa kupitia zawadi. Hii haimaanishi kuwa ni watoto wa tamaa au wanaopenda vitu vya gharama.

Kwa mujibu wa Gary Chapman, kwa watoto hawa zawadi ni ishara inayoonekana ya upendo na kumbukumbu kuwa mtu aliwafikiria.

Zawadi inaweza kuwa pipi ndogo, ua lilochumwa njiani, kalamu wanayoipenda au ujumbe wa mkono. Kinachogusa moyo wao si thamani ya fedha, bali maana ya zawadi hiyo.

Hata hivyo, wataalamu wanaonya kuwa zawadi haziwezi kuchukua nafasi ya uwepo wa mzazi. Wazazi wengine hujaribu kufidia kutokuwa karibu kwa kununua vitu vingi, lakini mtoto bado akahisi upweke wa kihisia.

## Matendo ya huduma (Acts of service)

Kwa watoto wengine, upendo unaonekana kupitia msaada wa vitendo.

Mzazi anayewasaidia kazi za shule, anayewafundisha kuendesha baiskeli au anayewatengenezea kitu kilichoharibika huwa anawafanya wajisikie cared for.

Gary Chapman anaeleza kuwa watoto hawa huona matendo ya huduma kama ishara ya kujaliwa na kuthaminiwa.

Lakini wataalamu wa malezi wanaonya kuwa huduma hizi zinapaswa kufanywa kwa moyo wa upendo, si kwa manung'uniko au hasira. Mtoto huhisi tofauti kubwa kati ya msaada unaotolewa kwa upendo na unaotolewa kwa kulazimika.




MAKALA
SAIKOLOJIA

UKHTI FATIMA SS

# Mazungumzo yanayojenga na yanayoharibu

Katika maisha ya kila siku, watu hutumia muda mwingi kuzungumza — kazini, nyumbani, kwenye ndoa, urafiki au katika uongozi. Lakini wataalamu wa saikolojia wanaeleza kuwa si kila mazungumzo huleta suluhisho. Baadhi hujenga mahusiano na maendeleo, huku mengine yakiongeza migogoro, hofu na ukimya.

Makala moja ya Psychology Today imeeleza aina nne za mazungumzo ambazo hujitokeza mara nyingi katika mahusiano na mazingira ya kazi: kulaumiana (blame), kukwepa tatizo (avoidance), kufuata mkumbo wa kundi (groupthink) na mazungumzo ya kusonga mbele (forward talk).

## Lawama: Kutafuta mkosaji badala ya suluhisho

Mazungumzo ya kulaumiana hutokea watu wanapokwama kwenye swali la nani mwenye kosa badala ya kutafuta suluhisho. Kauli kama "Nani aliharibu?", "Nani alikosea?" au "Tatizo hili ni la nani?" huonekana kuwa za kawaida, lakini mara nyingi huongeza ulinzi wa kihisia (defensiveness) na kufanya watu waogope kusema ukweli.

Katika mazingira ya kazi, utamaduni wa kulaumiana unaweza kuwafanya wafanyakazi kuficha makosa au kuogopa kutoa mawazo mapya. Katika ndoa au urafiki, kulaumiana hujenga hasira na umbali wa kihisia.

Wataalamu wa saikolojia wanasema mazungumzo ya aina hiyo huwafanya watu wajikite kwenye yaliyopita badala ya kutafuta namna ya kusonga mbele.

## Kukwepa tatizo: Ukimya unaokuza migogoro

Aina nyingine ya mazungumzo ni kukwepa tatizo. Hii hutokea pale watu wanaposema, "Tuongelee baadaye," "Mtu mwingine atalizungumzia," au "Tusifungue mjadala huo."

Kwa nje huonekana kama njia ya kulinda amani, lakini ndani yake tatizo huendelea kukua kimya kimya. Wataalamu wa afya ya akili wanaeleza kuwa watu wengi hukwepa mazungumzo magumu kwa sababu ya hofu ya migogoro, kukataliwa au kuumiza wengine.

Lakini matatizo mengi ya mahusiano huanza pale watu wanapoamua kunyamaza kwa muda mrefu. Hisia zisizosemwa mara nyingi hugeuka hasira, maumivu au umbali wa kihisia.

## Fikra za kundi: Wote hawaridhika, wote hawasemi

Pia kuna kile kinachoitwa groupthink — hali ambayo watu ndani ya kundi wanaonekana kukubaliana kwa nje ilhali ndani wana mashaka au hawaridhiki.

Mara nyingi watu hunyamaza ili wasiingie kwenye mgogoro au waonekane tofauti na wengine. Katika mikutano ya kazini, familia au hata jamii, hali hiyo inaweza kusababisha maamuzi mabaya kwa sababu watu wanaogopa kutoa maoni tofauti.

Wataalamu wa saikolojia wanasema mazingira ambayo watu hawawezi kupinga mawazo bila kuonekana wabaya huua ubunifu, ukweli na uwezo wa kuona hatari mapema.

## Mazungumzo ya kusonga mbele: Kujadili tatizo bila kuharibu watu

Aina ya nne ndiyo inayopendekezwa zaidi — forward talk au mazungumzo ya kusonga mbele.

Haya si mazungumzo ya kujifanya wapole kupita kiasi au kufunika matatizo. Badala yake, ni mazungumzo yanayolenga tatizo halisi huku yakitafuta suluhisho la baadaye.

Kwa mfano, badala ya kuuliza "Nani mwenye kosa?" mtu anaweza kuuliza, "Tunawezaje kuhakikisha hili halijirudii?" Badala ya kukwepa tatizo, watu hukubali kulijadili kwa uwazi lakini kwa heshima.

Wataalamu wa saikolojia wanaeleza kuwa mazungumzo ya kusonga mbele hujenga kile kinachoitwa psychological safety — mazingira ambayo watu wanahisi wako salama kusema ukweli bila kuogopa kudhalilishwa au kusham-